**CHADEMA** yawabana Spika, NEC vielelezo sakata la kina Mdee
UKURASA 4



**MWINYI:** Hii ndiyo siku niliyokasirika sana nikiwa Ikulu
UKURASA 3


Tuendelee kukatakata mikoa kweli?
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
SUA- TAWI MIZENGO PINDA Nuru mpya utalii, ufugaji nyuki na kilimo Nyanda za Juu Kusini
DK. KALEMANI ALIPOJINASIBU MANYARA REA IMEFIKISHA UMEME KILA UPENYO

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Mei 21, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580587

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# LUKU HASARA

**WAJASIRIAMALI** walia bidhaa kuharibika, Majaliwa apigilia nyundo TANESCO... *Endelea Ukurasa 2*

## HARUFU NEEMA BOMBA MAFUTA SASA YANUKIA

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na mgeni wake, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, baada ya kuwasili viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam jana, na baadaye kushuhudia utiaji saini mkataba wa nchi hodhi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## SIMANZI YATAWALA BUNGE KUPOTEZA MBUNGE MWINGINE

SIMANZI imetawala bungeni jana kutokana na taarifa za kifo cha Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Khatib Said Haji, aliyefariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili...

UKURASA WA 5

## MAJALIWA AWAONYA VIONGOZI WANAONYANYASA WAANDISHI



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameonya viongozi wa serikali wanaowaonea na kuwanyanyasa waandishi wa habari wanapokuwa katika...

## MSAKO UTAPELI 'TUMA NAMBA HII' KURINDIMA

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA - UBINGWA BARA TUTAUBEBA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Harufu neema bomba la mafuta sasa yanukia

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Rais Uganda, Yoweri Museveni, wamesema mradi wa bomba la mafuta la kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga utakapokamilika utakuwa kivutio cha wawekezaji wengi wa kimataifa kuja kuwekeza ukanda wa Afrika Mashariki na kutoa ajira nyingi.

Marais hao kwa nyakati tofauti walitaja faida za mradi huo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa utiaji saini utekelezaji wa ujenzi wa bomba hilo la kusafirisha mafuta ghafi unaogharimu kiasi cha Dola za Marekani bilioni 3.5.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Samia alisema manufaa ni pamoja na ajira kwa Watanzania na kuchochea utafutaji wa mafuta wa pamoja katika eneo la Afrika Mashariki.

Rais Samia alisema Tanzania itanufaika nao kwa sababu kati ya kilometa 1,443 za bomba hilo, kilometa 1,147 zitapita ndani ya mikoa minane na wilaya 24 nchini.

"Ajira nyingi zitazalishwa Tanzania, kama mnavyofahamu lipo deni la kuzalisha ajira zaidi ya milioni saba kwa miaka mitano ambazo tunaamini mradi huu utazichangia," alisema.

Rais Samia alisema mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kusafirisha mapipa ya mafuta bilioni 6.5 huku idadi ikitarajiwa kuongezeka kwa kuwa ugunduzi kimkataba ni asilimia 40, lakini zipo asilimia 60 zinaendelea kufanyiwa kazi Uganda ambazo wanaamini zitaingia kama sehemu ya mradi.

"Hatua hii itaongeza mapato mengi kwenye nchi zetu. Mathalani Tanzania, mbali ya gawio la kuwa na hisa kwenye kampuni, kama ilivyosemwa hapa tumeingia kwa kiasi chote tulichomegewa asilimia 15," alisema.

Mkuu huyo wa nchi alisema mbali ya asilimia hizo, watapata asilimia 60 ya faida ya mapato ya kodi ambayo Uganda watapata asilimia 40.

"Tatu, utachochea shughuli za utafutaji mafuta na gesi kwenye eneo la Afrika Mashariki, kama mnavyofahamu mbali ya mafuta yaliyogunduliwa Uganda, hapa Tanzania kuna mafuta yamegundulika, tuna mategemeo hayo," alisema.

Alisema ukiacha Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) nao wana tegemeo la kuyapata na miundombinu itakayotumika kusafirisha mafuta yote ni hiyo waliyotia saini.

Rais Samia alitoa wito kwa pande zote kuhakikisha zikamilisha majadiliano ya mikataba iliyobaki ili mradi huo uanze kutekelezwa na hatimaye ifikapo mwaka 2025 mafuta yaanze kusafirishwa.

"Wananchi wamesikia maneno haya kwa miaka mitano nyuma hivyo, maneno yaachwe mkatekeleze," alisihi.

Alisema shukrani ziende kwa Hayati John Magufuli ambaye alishirikiana na Rais Museveni kuhakikisha mradi unatekelezwa.

Rais Museveni alisema mradi wa bomba la mafuta ni sehemu ya miundombinu na kusisitiza kuwa, wananchi wa Tanzania na Uganda wasibweteke na kulewa nao na kusahau sekta zingine.

Rais Museveni alisema tukio hilo ni la kihistoria na kuipongeza Tanzania na Rais Samia kwa hatua hiyo muhimu na kuwashukuru mawaziri na maofisa wengine walioshiriki wakiwamo wataalamu waliopewa mafunzo na kugundua mafuta hayo Uganda.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), makao makuu ya zamani ya shirika hilo, Ubungo jijini Dar es Salaam, jana. Kulia ni Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani. **PICHA: OWM**

# Wajasiriamali walia hasara Luku

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wajasiriamali wamesema wamepata hasara kubwa kutokana kuharibika kwa mfumo wa Luku katika malipo ya huduma ya umeme.

Kutokana na adha hiyo, wameitaka serikali kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kutenga vituo vya ziada vitakavyowezesha kutoa huduma pindi inapotokea dharura kama hiyo.

Omary Pachaa na Amina Masudi, wakazi wa Mtaa wa Surugai, Kata ya Ipagala jijini Dodoma, waliiambia Nipashe jana kuwa kuwapo kwa vituo hivyo kutasaidia kuondoa adha ambazo wananchi wamepata.

"Shirika limewatia harasa ya mamilioni ya shilingi Watanzania kutokana na walio wengi kutumia huduma hiyo kibiashara zaidi, hivyo ni wakati sasa kwa TANESCO (Shirika la Umeme) kujiongeza," walisema.

Bakari Hassan, mjasiriamali mwenye duka la samaki na maziwa katika Mtaa wa Swaswa, Ipagala jijini Dodoma, alibainisha kuwa katika kipindi cha siku tatu ambazo huduma ya Luku ilikosekana, amepata hasara kubwa kutokana na kuharibika kwa bidhaa hizo.

Hassan ameiomba TANESCO kuhakikisha wataalamu wake wanasimamia maeneo muhimu kama vile mfumo huo.

Mariam Bakari, mkazi wa Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, alisema hawakupewa ushirikiano na watoa huduma wa shirika kwenye ofisi za TANESCO zilizoko karibu na makazi yao.

"Usiku wa jana (juzi) tulikuwa wengi katika kituo kile na askari wa ulinzi walikuwa wanatufukuza, tuligoma kuondoka na tukamtaka meneja wa kituo aje kutupa maelezo na alipokuja alituambia kuwa kituo hicho hakitoi huduma ya kuuza umeme, hivyo tuende makao makuu," alisema.

Wakati wananchi wakibainisha hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ametaka uchunguzi zaidi ufanyike kuhusu kukosekana kwa huduma ya Luku kwa siku tatu huku akiagiza waliosimamishwa kwa siku 10 waendelee kusimama mpaka utakapokamilika.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana mkoani Dar es Salaam baada ya kwenda makao makuu ya zamani ya TANESCO na kukutana na uongozi na Bodi ya Wakurugenzi.

Juzi, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipokwenda TANESCO, aliagiza Meneja wa Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA) na Huduma za Biashara wa shirika hilo, Lonus Feruzi na wasaidizi wake, Frank Mushi na Idda Njau, wasimamishwe kwa siku 10 kupisha uchunguzi na endapo hawatakutwa na hatia warudhishwe kazini.

Majaliwa alimwagiza Waziri Kalemani badala ya kuwasimamisha kwa siku 10, wakae pembeni hadi uchunguzi utakapokamilika.

"Umewasimamisha siku 10 kama uchunguzi unakuwa haujakamilika warudi kazini tena, watarudi tu pale ambapo tutajiridhisha hili jambo lipo vizuri.

"Miaka yote walikuwa wanajua hiki kitu ni cha kudumu, sasa kimeharibika chini ya usimamizi wao siku tatu wamesumbua wananchi.

"Mkurugenzi Mkuu wa shirika unaona kilichotokea, Bodi ya Wakurugenzi si mmeona? Huu uwajibikaji usiishie hapo, lazima uende mbali zaidi.

"Kama sisi wakurugenzi mlijua kuna mfumo huu na lazima tujihakikishie unakwenda vizuri halafu itakapotokea umeshindwa kufanya kazi lazima tuwe na mtambo ambao utapokea kuendelea kutoa huduma lakini hainunuliwi wakati nyie ndiyo mnatengeneza bajeti na kujua mahitaji ya shirika, tunafanyaje, ni muhimu kujitathmini, watendaji wote wa sekta," aliagiza.

Majaliwa amesema tukio hilo limetikisa serikali na kuleta usumbufu mkubwa kwa wateja baada ya kukosekana kwa huduma na katika siku hizo tatu ulikuwa ukikatika.

"Unakatika unapoteza mawasiliano baadaye unarudi unakatika tena baadaye unarudi matukio ambayo hatujayazoea kwa kipindi kirefu tulisimamia vizuri mifumo yetu huduma za umeme zinaendeshwa vizuri," alisema.

Majaliwa alisema lengo wanataka kupata taarifa kwa nini wamesababisha mtikisiko ndani ya serikali kwa kutotekeleza majukumu ambayo yameleta tatizo hilo.

"Miaka mingi nyuma tulikuwa tunapata tatizo kubwa la umeme na huduma hii tulikuwa tunapata kwa watu binafsi, serikali ikafanya marekebisho makubwa kuhakikisha huduma inasimamiwa na serikali kwa ujumla ili kuondoa maslahi ya mtu mmoja mmoja kwa makusudi anaamua kuharibu ili kuwe na kero," alisema.

Alisema lazima wananchi wapate maelezo kwa nini umeme haukupatikana kwa siku zote wakati wao ndiyo wanasimamia kwenye maeneo yote ya Luku.

"Uamuzi uliofanywa awali na serikali wa kusimamia maeneo nyeti ya huduma, eneo hili bado shirika hamkutaka kulikamilisha lote, suala la mfumo hakukuwa na sababu mtu mwingine ausimamie, anapotaka kuwasumbua mtayumba, mbona kipindi chote tumekwenda na tumefanya vizuri?" Alihoji.

Majaliwa alisema mifumo yote imetengenezwa inapopata tatizo inakuwa na kitu kingine inaanza mara moja kazi ile ile ili isiyumbe lakini taarifa tulizonazo mfumo huo hauna mtambo huo.

"Mmetengeneza usumbufu mkubwa, mmewafanya wateja wazungumze maneno mengi mengine hatuwezi kuyatamka, tukisema ni wa makusudi mtabisha, na ikitokea miongoni mwenu akiamua kuzima kwa makusudi kusumbua tu mtasema nini?

"Mwenyekiti wa bodi hujui haya miaka yote ya kwamba mlitakiwa mtenge fedha kununua mtambo huu?" Majaliwa alihoji.

- **Imeandikwa na Peter Mkwavila (DODOMA), Maulid Mmbaga na Romana Mallya (DAR ES SALAAM)**

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Afrika, Dk. Weggoro Nyamajeje (wapili kulia), aliyeambatana na Kaimu Ofisa Mtendaji wa benki hiyo, Wasia Mushi na Ofisa Mwandamizi wa benki hiyo, Samir Yassine, Ikulu mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhakiki laini za simu kukabili uhalifu mbioni

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema kuwa serikali inaandaa utaratibu wa kuhakiki laini za simu nchini na zitakazobainika kutumika ndivyo sivyo zitafungiwa.

Uamuzi huo ni katika kupambana na uhalifu mtandaoni ambao kwa sasa umeshika kasi nchini na wabunge wanne kueleza jinsi walivyotapeliwa huku wakiomba serikali kuchukua hatua.

Alisema hataki kukumbukwa kama waziri aliyeongoza sekta kama polisi bali aliyeleta mageuzi yaliyogusa maisha ya watu wengi. Akifanya majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/22 bungeni jana, Ndugulile alisema watafanya mabadiliko makubwa ya sheria zinazosimamia sekta hiyo.

"Nimejielekeza zaidi katika kutoa elimu kuliko kukamata watu, nimebaini wengi hawana uelewa wa teknolojia na hawajui sheria hivyo wanatumia ovyo mitandao, sitaki kuwa waziri wa kukamata bali wa kuelimisha zaidi maana hiyo mbinu haijafanikiwa," alisema Ndugulile.

Alisema serikali inataka kuachana na kukata kodi kwenye 'Youtube' ambazo wasanii wanarusha kazi zao au washereheshaji wanarusha kazi zao mtandaoni.

"Unamtoza kodi mtu karusha mtandaoni kazi yake ya MC au wimbo wake, huku ni kuua kazi zao, tunataka tuondoke huko," alisisitiza.

Pia alisema maboresho ya sheria ya kulinda faragha ipo mbioni na lengo siyo kuminya uhuru wa watu kujieleza na kutumia mitandao, bali kulinda taarifa za watu kutotumika ovyo duniani.

Akiwasikisha makadirio ya wizara yake, Waziri Ndugulile alisema, laini za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka 48,939,530 mwaka 2020 hadi kufikia laini 53,063,085 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 10.8.

Aidha, watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka 26,832,089 mwaka 2020 hadi kufikia 29,071,817 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 8.3.

Waziri Ndugulile alisema laini za simu kwa njia ya kibiometria nchini hadi kufikia mwezi Aprili 2021, jumla ya laini 51,108,886 za simu ambazo zimesajiliwa kwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi na kitambulisho cha mpigakura ni 1,954,199 na kufanya jumla ya laini ambazo zimeunganishwa na mtandao kufikia 53,063,085.

# Kortini tuhuma wizi mil. 800/- kituo cha mafuta

**Na Hellen Mwango**

MABOSI wawili wa kituo cha mafuta cha Sasa Kazi mkoani Dar es Salaam, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na tuhuma za kula njama na wizi wa zaidi ya Sh. milioni 852 mali ya mwajiri wao.

Washtakiwa hao ambao ni wasimamizi wa kituo, Najib Masoor na Shadya Joseph, walifikishwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai katika shtaka la kwanza, wakiwa ni watumishi wa kituo hicho cha mafuta kilichopo eneo la Mtoni Mtongani, Wilaya ya Temeke, walikula njama ya wizi kati ya Januari Mosi, 2018 na Machi 26, 2020.

Alidai pia katika shtaka la pili wakiwa watumishi wa kituo hicho waliiba Sh. 852,246,698, mali ya mwajiri wao.

Jamhuri ilidai upelelezi haujakamilika, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu Chaungu, aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili kila mmoja watakaosaini hati ya dhamana yenye thamani ya Sh. milioni 200.

Pia mahakama iliwataka washtakiwa kutoa Sh. milioni 220 taslimu kila mmoja au hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Hata hivyo, Mshtakiwa Mansoor alitimiza masharti ya dhamana wakati Shadya alipelekwa mahabusu, baada ya kushindwa kutimiza masharti hayo. Kesi hiyo imepangwa kutajwa Juni 3, 2021.

# Mwinyi: Hii ndiyo siku niliyokasirika sana

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha kuwa Februari 10, 1995 ndiyo siku aliyokasirika zaidi katika uongozi wake Ikulu.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema kuwa siku hiyo aliitisha kikao na vyombo husika kuzungumzia biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Anasema biashara ya dawa za kulevya ilikuwa imepamba moto kiasi cha kuhitaji ushirikiano wa kimataifa katika kupigana nayo.

"Waliokamatwa kwa kiasi kikubwa ilikuwa kama bahati tu au kwa msaada wa raia wema na si kwa mbinu za uhakika na maalum za vyombo vya serikali.

"Maana ingawa niliwapongeza waliohusika na kukamatwa, bado nilihisi tunagusagusa tu, hatukuwa tumefika kwenye kiini cha tatizo na mbinu za kulikomesha," anabainisha. Anasema kuanzia mwaka 1988 hadi 1990 kulikuwa na matukio 50 tofauti ya watu waliokamatwa wakiwa na dawa za kulevya aina ya Heroin na Morphine katika nchi nzima na mmojawapo alikamatwa na kilo 2.3 za heroin safi.

"Kuanzia mwaka 1983 hadi 1991, jumla ya watu 358 wenye pasipoti za Tanzania walikamatwa nchi za nje kwa kutumia, kusafirisha au kuuza dawa za kulevya.

"Mwezi Oktoba, 1991 lilikamatwa kontena moja la futi 20 likiwa na tani 5.6 za bangi, huku wenye nalo wakidai walikuwa wanasafirisha nguo za pamba. "Mwezi Desemba 1991, kinamama wawili wa Kifaransa walikamatwa maeneo ya Posta Kuu ya Dar es Salaam wakijaribu kupeleka nje ya nchi kwa njia ya posta gramu 100 za bangi iliyokuwa imefichwa ndani ya kopo la kahawa.

"Mwezi Mei 1991, mtu mmoja raia wa Korea ya Kusini alikamatwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam akiwa na heroin.

"Mwezi Mei 1993, mwanamke mmoja raia wa Kenya alikamatwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro akiwa na kilo 3.7 za heroin yenye thamani ya Sh. milioni 234 wakati ule sawa na Dola 585,000.

"Mwezi Agosti 1993, Nurdin Akasha, alikamatwa akiwa na tani 1.1 za dawa za kulevya aina ya mandrax yenye thamani wakati ule ya Sh. bilioni 4.988 sawa na Dola milioni 11.36 na akafikishwa mahakamani na kushtakiwa. "Agosti 18, 1993 dereva mmoja wa lori alikamatwa Mbeya akiwa na kilo 488.6 za mandrax.

"Septemba 21, 1993 dereva mwingine wa lori alikamatwa Tanga akiwa na kilo 161 za mandrax. Mwaka 1994 dereva mwingine wa lori alikamatwa Msamvu Morogoro akiwa na vidonge vingi sana vya mandrax.

"Katika miezi saba ya mwanzo ya mwaka 1992 kulikuwa na matukio 997 ya watu kukamatwa wakiwa na dawa za kulevya ndani ya Tanzania, yaani wastani wa watu 142 kila mwezi.

"Asilimia 72 walikuwa vijana wa umri kati ya miaka 15 na 30 huku karibu asilimia 40 yao wakiwa wanawake.

"Mwezi Januari 1995, vijana watano wa Kitanzania walikamatwa kwenye viwanja vya ndege vya Zanzibar na Dar es Salaam wakiwa wamemeza zaidi ya paketi 70 za heroin wakiziita pipi enzi hizo," anakumbusha.


PMM ESTATES (2001) LTD
Inland Container Depot (ICD)
ICD No. 0015
Nyerere Road, Plot No. 2384/75
P.o Box 33790, Dar es salaam, Tanzania
Telephone: +255 222863669 / 2863670

**We are hiring a TYRE TECHNICIAN:**

We are looking to hire an experienced Tyre Technician for our busy workshop, transport, and equipment operations.

The role of the Technician is making sure that tyres used by vehicles and equipment are in good state.

**Responsibilities:**

- Conduct daily tyre and related inspection
- Check and maintain proper tyre inflation
- Assess worn and damaged tyres, tread levels, wear pattern, valve quality, and overall health
- Repair or replace faulty tyres and valves
- Supervise balancing and alignment
- Conduct timely tyre rotation
- Maintaining detailed tyre records and files
- Maintaining and Safe keeping tyre tools, equipment, and spare tyres in your stock
- Planning, reporting, and advising
- Assigning and supervising works to your subordinates
- Maintain and Abide to the tyre regulations and all company policies
- Perform any other duties assigned by your senior staff

**Requirements:**

- College education
- Knowing different types of tyres, tubes, rims and accessories
- Ability to display professionalism
- Maintaining quality focus
- Attention to detail
- Skills on the construction of tyres
- Have tyre removal and fitting techniques
- Knowledge of tyre working tools and equipment
- Ability to work with some computer office applications
- Working healthily and safely
- Physically fit

**How to apply:**

**Send your application before 7th June, 2021 to:**
**HRM,**
**PMM Estates (2001) Ltd,**
**P.O.Box 33790 DSM**
**hrm@pmmicd.co.tz**

## Jaji Mkuu ahimiza matumizi ya TEHAMA kwa mahakama

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JAJI Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma, amewataka mawakili na watumishi wa mahakama nchini, kujenga utaratibu wa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kazi zao ili wasiachwe na teknolojia hiyo.

Pia, alisema wanahitaji kuona ubebaji wa mafaili ya kumbukumbu wakati wa mikutano mbalimbali unapungua kwa kuyahifadhi katika mfumo wa kielektroniki.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Mahakama nchini, alisema kuna baadhi ya kada katika mahakama zinaweza kukosa kazi kutokana na utandawazi ambao utasababisha kazi nyingine kufanywa kwa njia ya kielectroniki.

Alisema lengo ni kuifikisha mahakama katika utoaji haki kwa njia ya mtandao na mifumo mbalimbali itatumika ikiwamo inayotumia mitandao na kwamba ni vyema kila mtumishi akajua kutumia teknolojia hiyo.

"Naomba tujenge utaratibu wa kutumia teknolojia ya TEHAMA ikiwamo kujifunza kila kitu, hivi sasa kinapatikana kupitia mitandao kama uliona

tukio la kukosekana kwa umeme watu wamejua kupitia mitandao," alisema Prof. Juma.

Alisema katika utoaji wa haki kwa njia ya mitandao kutakuwa na mifumo mbalimbali itakayotumika na kutakuwa na usimamizi wa mashauri wa kielektroniki.

Pia, mfumo wa usimamizi wa mali wa kielektroniki, mfumo wa usimamizi wa nyaraka wa kielektroniki na mfumo wa usimamizi wa utunzaji kumbukumbu wa kielektroniki.

## BAWACHA yawabana Spika, NEC vielelezo vya kina Mdee

**Na Richard Makore,** MWANZA

BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limemtaka Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, kutoka hadharani na vielelezo ikiwamo fomu namba 8 kama uthibitisho aliotumia kupeleka majina 19 ya wabunge wa CHADEMA kula kiapo bungeni.

Kadhalika, BAWACHA imemtaka Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuheshimu katiba kwa kuwaondoa bungeni wabunge 19 wa CHADEMA kwa kuwa wapo huko kinyume cha katiba.

Akizungumza katika kikao cha kamati tendaji ya BAWACHA kilichomalizika jana jijini Mwanza, Kaimu Mwenyekiti wa baraza hilo, Sharifa Selemani, alisema wamechoka kuona katiba ikiendelea kuvunjwa.

Alimtaka Dk. Mahera kujitokeza akiwa ameshikilia fomu namba 8 na kuonyesha umma nani aliisaini kwa kuwa wanaamini nyaraka hiyo ilighushiwa.

Sharifa alisema baraza hilo linakusudia kuandamana kushinikiza wabunge hao 19 waondolewe bungeni kwa kuwa hawapo huko kwa baraka za chama.

Kuhusu Spika kuendelea kuvunja katiba, Sharifa alisema kuna ushahidi wa wazi kwamba kulikuwa na njama mbaya za kuwapeleka bungeni wabunge ambao hawakuteuliwa na chama kupitia barua rasmi.

Spika Ndugai kwa nyakati tofauti amenukuliwa akisema wabunge 19 waliofukuzwa uanachama na CHADEMA ni wabunge kamili labda wao wenyewe waamue kwa kutumia utaratibu wa kikatiba kujiuzulu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema Kamati Kuu ya chama hicho iliridhishwa na ukweli kwamba kuna ukiukaji mkubwa wa katiba ya nchi, sheria za nchi na kanuni zinazosimamia masuala ya uchaguzi zilizokiukwa katika mchakato mzima wa uchaguzi huo, hususani katika jambo zima linalohusu viti maalum.

"Tumejiridhisha katika uvunjaji huu wa katiba, sheria na kanuni kama kamati kuu ya chama cha upinzani CHADEMA, lazima tulifahamishe taifa baada ya kujiridhisha sisi wenyewe baada ya vikao vya ndani va chama kuhusu mapungufu kadhaa yaliyofanyika katika mchakato huu."

Mbowe aliainisha mapungufu ya kisheria aliyosema yako dhahiri katika mchakato wa uteuzi wa wabunge wa viti maalumu kuwa ni Ibara ya 78 (3), inayosema majina ya watu waliopendekezwa na Tume ya Uchaguzi yatatangazwa kama matokeo ya uchaguzi, baada ya tume kuridhika kwamba masharti na sheria vimezingatiwa.

Ibara ya 67 (1b) imeweka masharti na sifa ya mtu kuteuliwa kuwa mbunge kuwa lazima awe amependekezwa na chama cha siasa.

Mbowe alisema kuwa mtu hawezi kupendekezwa na chochote kingine kwa mujibu wa sheria za nchi, isipokuwa na chama cha siasa.

## Bunge lapoteza mbunge mwingine

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIMANZI imetawala bungeni jana kutokana na taarifa za kifo cha Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Khatib Said Haji, aliyefariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alikokuwa akipatiwa matibabu.

Hali hiyo ilijitokeza baada ya Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutangaza taarifa za msiba huo bungeni na kuahirisha shughuli za Bunge zilizopangwa kufanyika jana hadi leo saa tatu asubuhi.

**BAJETI YAAHIRISHWA**

Shughuli zilizopangwa kufanyika jana ni pamoja na kipindi cha maswali na majibu kwa wabunge na hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2021/22.

Akitoa taarifa ya Spika kwa Bunge kuhusu kifo hicho, Dk. Tulia alisema "Mheshimiwa Spika kwa masikitiko makubwa sana anawatangazia waheshimiwa wabunge na kuwataarifu kwamba mbunge mwenzetu, Khatib Said Haji wa ACT-Wazalendo amefariki leo (jana), majira ya saa 11:40 alfajiri katika Hospitali ya Muhimbili alipokuwa akipata matibabu."

Alisema maziko yake yamefanyika jana saa 10 alasiri Kisiwani Pemba.

Alisema Bunge litawakilishwa na baadhi ya wabunge ambao walikuwa Dar es Salaam kwenye shughuli ya kitaifa ya utiaji saini utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta. "Kwa taratibu zetu kwa wale ambao wapo kule basi wataangalia uwakilishi wa vyama humu ndani na uwakilishi wa mambo mengine kama ambavyo huwa tunafanya katika taratibu zetu," alisema.

Kutokana na kifo hicho, Naibu Spika huyo, alisema kwa mujibu wa kanuni ya 173, inataka kuahirisha shughuli za Bunge inapotokea kifo cha mbunge wakati likiwa katika shughuli zake.

"Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho (leo) Ijumaa tarehe 21, Mei mwaka 2021 saa tatu kamili asubuhi ili waheshimiwa wabunge wapate muda wa maombolezo kwa ajili ya huyu mwenzetu," alisema.

**WAMZUNGUMZIA MAREHEMU**

Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambaye ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema mbunge huyo alikuwa mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na alikuwa akitoa michango mikubwa kwenye kamati hiyo.

"Michango yake ilikuwa ni muhimu sana maana ni mtu ambaye alikuwa akisimama na kutoa hoja na mambo mengi ambayo tunafanya sisi kama wizara ili kutekeleza azma ya kuwa na uchumi unaoendeshwa na viwanda ni kutokana na michango yake, kwa sababu na yeye alikuwa mdau mkubwa sana wa biashara ikihusisha shughuli ambazo zinafanywa na wananchi wote."

Naye Mbunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Bakar Ahmad Bakar, alisema Khatib alikuwa mkarimu na mwenye mashirikiano makubwa.

"Tulikuwa tunashirikiana naye pamoja na kuwapo kwa utofauti wa vyama, hilo hatukulijali yeye wakati wa kazi ni kazi wakati wa ushirikiano tulikuwa tunashirikiana, alikuwa anatoa maoni yake kwa namna ambavyo anaona inafaa na mara ya mwisho maoni yake ilikuwa masuala ya mashekhe wale Uamsho."

"Nadhani nakumbuka kitu kama hicho alikuwa anawapigania kwa vile wamekaa sana pale mahabusu alikuwa anapigania wapatiwe haki zao kama wanashtakiwa washtakiwe na kama sio wa kushtakiwa basi waruhusiwe warudi nyumbani, nadhani huo ndio ulikuwa mchango wake wa mwisho," alisema.

Alisema kutokana na kusumbuliwa na maradhi mara ya mwisho Mbunge wa Mtambwe (ACT-Wazalendo), Khalifa Mohamed Issa, alimuulizia swali lake bungeni Mei 17, mwaka huu.

"Tutamkumbuka kwa misimamo yake, alikuwa ni mtu wa misimamo alikuwa anasimamia kile ambacho anakiamini kuwa ndivyo kilivyo," alisema.

**SWALI LAKE LA MWISHO**

Katika swali lake la msingi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lililoulizwa kwa niaba yake na Mbunge Khalifa, Mbunge huyo aliyehoji mkakati wa serikali kukabiliana na manabii na waganga matapeli.

"Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uongo wanaodanganya na kuwatapeli wananchi kila siku."



HABARI KITAIFA

# Majaliwa awaonya viongozi wanaonyanyasa waandishi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameonya viongozi wa serikali wanaowaonea na kuwanyanyasa waandishi wa habari wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yao kuacha tabia hiyo mara moja na watakaoendelea kufanya hivyo watachukuliwa hatua kali.

Alisema sera ya serikali sio kuwaonea waandishi wa habari na haitamvumilia kiongozi au mtu yeyote atakayemkwaza mwandishi wa habari akiwa katika kazi ya uandishi. Pia aliwahakikishia waandishi wa habari kuwa serikali itaendelea kuimarisha misingi ya habari nchini.

Alitoa onyo hilo, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), mjini Morogoro na Kongamano la Kitaaluma (Editors Retreat), pamoja na uchaguzi wa viongozi watakaongoza katika kipindi cha miaka minne.

Alisema serikali inawatambua na kuwathmini waandishi wa habari kutokana na kazi yao kubwa ya kuchochea shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na serikali na isingependa kuona mwandishi anapata tatizo anapotimiza wajibu wake.

"Mchango wenu waandishi wa habari ni mkubwa mno na serikali inautambua kwa kuwa mmekuwa mkisaidia kuchochea katika shughuli za maendeleo hivyo kama serikali tusingependa kuona kuna mtu anawaonea wakati wa kutimiza wajibu wenu," alisisitiza.

Alisema Tanzania ni moja ya nchi katika Afrika ambazo zinaongoza kuwa na vyombo vingi vya habari ikiwamo magazeti, radio, television na TV mtandaoni kutokana na kutambua mchango mkubwa unaofanywa na vyombo vya habari kwa mshikamano wa kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

"Waandishi wa habari ni watu muhimu sana na sisi kama serikali tutaendelea kuwatumia, na kuwatumia huku kunatokana na thamani ya mchango mnaotoa, tutahakikisha mnalindwa mnapokuwa mnatekeleza majukumu yenu ya uandishi wa habari," alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na ushirikiano huo, aliwataka kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni, weledi na kutanguliza uzalendo wa taifa lao kwa kuwa hawana nchi nyingine isipokuwa Tanzania.

Akizungumzia uhuru wa vyombo vya habari, aliwataka waandishi kuzingatia sheria za nchi, wasitumie vibaya kalamu zao kwa kumwonea mtu na itumike katika kusimamia haki ya kila mmoja.

Alisema serikali kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeweka bayana mpango wa kuboresha mazingira ya wanahabari nchini na kuhakikisha uhuru wa kupata habari na kutoa habari unaendelea kutekelezwa kwa mujibu wa sheria.

Akijibu hoja ya Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, kuhusu madeni ya serikali yanayodaiwa na vyombo vya habari na kusababisha hali mbaya ya kiuchumi kwenye vyombo hivyo, Waziri Mkuu aliagiza vyombo vya serikali, wizara na taasisi zinazodaiwa ifikapo Juni 30, mwaka huu ziwe zimeshalipa madeni yake.

Aliiagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuweka mpango na mkakati wa kushirikisha vyombo vya habari kikamilifu na kuharakisha mchakato wa kuundwa bodi ya ithibati itakayofanya kazi ya kusimamia maadili ya taaluma ya habari na kuwezesha kuwa na baraza huru la habari.

Awali Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema tayari kuna maazimio yaliyotolewa kwenye siku ya uhuru wa vyombo vya habari nchini na kama wizara wapo tayari kuyapitia na kufanya maboresho sehemu zenye changamoto kwa waandishi wa habari.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Balile, aliomba viongozi wa kitaifa kama Rais, Makamu na Waziri Mkuu kuwa na utaratibu wa kukutana na wahariri na waandishi wa habari kwa ajili ya kujadililiana kuhusu maendeleo ya nchi kwa manufaa ya Watanzania.

# CCM yataka ukurasa mpya wa siasa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewahimiza wanasiasa nchini kufungua milango ya utengamano, maelewano na siasa zenye mashiko kwa mstakabali wa taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe kushika nafasi ya Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema dhamira ya CCM bado ipo palepale kuhakikisha haishiriki siasa za mti kwa macho, piga nikupige, au watu kuhasimiana kwa sababu za kisiasa.

"Hivyo tunawahimiza wanasiasa wenzetu, kufungua milango ya utengamano maelewano na siasa zenye mashiko na mantiki kwa mstakabali wa taifa," alisema.

Alisema chama hicho kinaahidi kufanya siasa safi zenye mashiko na kubeba mstakabali wa taifa katika kuwaunganisha Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao.

Katika hatua nyingine, Chongolo alisema CCM imetoa maelekezo mahususi katika bajeti ya mwaka 2021/22 kwa wizara tatu ambazo ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Nishati na Kilimo huku ikitoa vipaumbele vinavyopaswa kuzingatiwa kwenye bajeti zao.

"Ni utaratibu wa chama kuisimamia serikali, leo tumetoa maelekezo hapa, sisi kazi yetu ni kusikiliza hotuba za bajeti zao za wizara kama hawataingiza vipaumbele tulivyoainisha hapa tutajuana huko mbele ya safari sisi tuna vikao vitakavyotuelekeza hatua za kuchukua."

"Sisi tunasubiria vikao kwa sababu tutarudisha kwao na tutakubaliana huko, kwa hiyo hili jambo sio la mchezo kwa sababu wapo pale kutimiza haya, wasipotimiza tutajuana namna nzuri ya kutimiza au watusaidie namna nzuri ya kuwa na watu watakaotimiza," alisema.

Katibu huyo alisema chama hicho kinaagiza serikali kupitia wizara yake kutatua migogoro ya ardhi iliyopo, kuthamisha ardhi ili kuziongezea tija, pamoja na kuhakikisha wananchi wamiliki ardhi kisheria ili kupunguza migogoro.


Enabel

## National Technical Advisor (m/f/x) – Kigoma Region,Tanzania

**Enabel is the Belgian development agency. It implements Belgium's governmental cooperation. The agency also implements actions for other national and international donors. With its partners in Belgium and abroad Enabel offers solutions addressing pressing global challenges: Climate Change, Urbanisation, Human Mobility, Peace and Security, Economic and Social Inequality, and Global Citizenship. With 1,500 staff, Enabel manages about 150 projects in twenty countries, in Belgium, Africa and the Middle East.**

**Background**

**The Water and Sanitation Kigoma Region Project** (WASKIRP) is a project focusing on water supply services sustainability in rural areas. In rural Tanzania and Kigoma region many water supply systems are mal functioning or out of order due to weak management, ageing infrastructures and lack of Operation and Maintenance (O&M) throughout time. As a consequence, a large part of the population is suffering from inadequate and intermittent water supply. For these reasons WASKIRP will be supporting the establishment of Community Owned Water Supply Organizations (COWSO) as well as improving existing infrastructures with a view of sustaining the water supply service in the long run. The project is aligned with national policies and strategies, contributing directly to the implementation of Tanzania Water & Sanitation Development Plan 2007-2020 (WSDP).

**Job Description**

The National Technical Advisor reports to the Project Manager.
Your tasks and responsibilities:

- You support design processes for upcoming water supply projects and in reviewing technical documents;
- You advise on the basis of your technical expertise in learning and capitalisation, in order to achieve performance in accordance with national norms and standards;
- You organise all site visits, linking up with communities and district-level stakeholders;
- You participate in missions and community engagements, preparing action points for the attention of the implementation unit;
- You facilitate participation of all stakeholders in identifying construction sites of water supply structures and in selection of technologies;
- You ensure the quality of all works under the program;
- You ensure the projects' compliance to environmental protocols;
- You work and facilitate effective catchment protection measures with Lake Tanganyika Basin Water Board;
- You take a leading role in building the capacity development of community-based water supply organizations;
- You support a Junior Expert and Rural Water and Sanitation Agency (RUWASA) in assessing technical capacity gaps of Community-Based Water Supply Organizations (CBWSOs);
- You facilitate and coordinate all activities relating to Environmental and Social Impact Assessment for Kakonko and Kidyama projects;You support Lake Tanganyika Basin Water Board to establish Water User Associations for Nyete in Kigoma rural district, Kivuruga in Buhigwe, Mkugwa in Kibondo;
- You support the Basin to carry out capacity strengthening activities for Mkuti in Uvinza and Mtunguruzi in Kakonko;
- You facilitate demarcations in the project to protection water supply structures like intakes, storage tanks and similar structures in Mkongoro, Mwayaya, Kasulu, Kakonko;
- You prepare quarterly budgets for technical activities of the program;
- You participate in evaluation of tenders and contractors and contribute to the evaluation reporting.

**Your profile**

**Required qualifications and experience**

- Bachelor's degree in civil/water or in any other relevant engineering discipline, from a recognized academic institution;
- At least 10 years of experience in water supply and sanitation;
- A professional experience in a Non-Governmental Organization/bilateral agency is an asset.

**Required skills and knowledge**

- Good knowledge of aspects of international development (context, challenges, application, partners, functioning…);
- Ability to use new technologies used in the area of water supply and sanitation;
- Pro-active results-oriented project management ;
- Excellent management and organisational skills ;
- Excellent synthesis, writing and analytical skills;
- Good knowledge of standard ICT applications;
- Good interpersonal and leadership skills;
- You show respect and are able to build relations on the basis of credibility and expertise;
- You show engagement, sense of responsibility and integrity;
- You are fluent in spoken and written English and Swahili.

Applicants are also required to commit to the vision, mission and values of Enabel (**https://www.enabel.be/content/enabel-vision-mission-values**).

**We offer**

- An interesting job in an international environment.
- A contract of 16 months . You are based in Kigoma. Occasional missions to the site in Kigoma region where we implement projects are possible.

A salary package that comprises the monthly gross salary, in accordance with our salary scales (Class 5), hospitalization/healthcare insurance, 13th month, double holiday allowance and reallocation allowance.

Following this recruitment procedure a shortlist of successful applicants may be constituted which may be sourced in the next three years for similar job openings.

***Every person who fulfils the conditions listed in our job advertisements may apply. Enabel is committed to equal opportunities and diversity in its workforce. We do not discriminate on the basis of gender, origin, age, religion, sexual orientation, disability status.***

**Are you interested?**

Apply at **www.enabel.be** the latest by 04/06/2021 and include your application letter and updated CV.

**Enabel • Belgisch ontwikkelingsagentschap • Naamloze vennootschap van publiek recht met sociaal oogmerk • Hoogstraat 147 • 1000 Brussel • T +32 (0)2 505 37 00 • enabel.be**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio hiki cha wizi mtandaoni hakitibiki?

**KWA** muda mrefu kumekuwa na kilio cha watu kutapeliwa fedha mtandaoni na watu ambao wamesajili namba kwa majina tofauti na sasa wabunge nao wamepaza sauti na kueleza namna walivyopigwa fedha. Juzi wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, wabunge wanne walitoa mfano wa 'kupigwa' fedha kwenye mitandao kwa kupigiwa simu kama zimetoka kwenye kitengo cha huduma kwa wateja cha kampuni ya simu na ile ya kutumiwa ujumbe mfupi kuambiwa 'ile fedha tuma kupitia namba hii'.

Wabunge hao walihoji kama usajili wa laini ulifanyika kielektroniki kwa alama za vidole, iweje watu waendelee kutapeliwa, na waliendа mbali zaidi kueleza kuwa wahusika walitafutwa na wanapokea simu hadi sasa na wote wamesajiliwa.

Walisema wananchi wanalizwa sana kwa kuwa matapeli hao wa mtandaoni wanatumia mbinu nyingi, lakini kinachoshangaza ni kwamba wote wamesajili laini kwa alama za vidole.

Kilio cha wabunge hao ni kiwakilishi na wananchi wengi ambao wanalia kutapeliwa, na kasi ya kusambaa kwa jumbe za 'tuma fedha kwa namba hii' au 'mwanao aliyeko shule fulani anaumwa sana kapelekwa hospitali' hivyo wasiliana na daktari utume fedha kinaongezeka. Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alizungumzia suala hilo kwamba wananchi wamesajili laini kwa alama za vidole, lakini bado wameendelea kutapeliwa na kulitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua. Katika majibu wa hoja za wabunge, Waziri wa Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alisema serikali inafuatilia kwa karibu na zaidi inajikita kutoa elimu ili wananchi watambue sheria, kanuni, taratibu na matumizi sahihi ya mitandao. Aidha, alisema serikali inatarajia kuanza uhakiki wa laini zote za simu nchini, ili kuzifuta ambazo zinatumika ndivyo sivyo, na kuchukua hatua kwa wanaofanya utapeli.

Haya yote yanafanyika kukiwa na kitengo cha makosa ya mtandaoni kwenye Jeshi la Polisi na wataalamu ambao wamepikwa katika Chuo cha Polisi Moshi (CCP) na vingine nchini, lakini bado wanaokamatwa siyo wanaotuma ujumbe au kupigia wateja simu.

Tunatambua zipo jitihada kadha wa kadha kama kutuma ujumbe kwa wananchi kupitia mitandao mbalimbali, kuwa wasikubali kutuma fedha kwa mtu wasiyemjua au wasitoe namba zao za siri kwa mtu yeyote, lakini bado utapeli unashika kasi.

Tunaiomba serikali kuangalia suala hili kwa kina na hasa kurudi kwenye lengo la kusajili laini kwa alama za vidole kuwa ni kupunguza au kumaliza matukio ya utapeli kwa kuwa mtu anayetenda haya atatambulika na kukamatwa kirahisi.

Pia, sheria imekataza mtu mmoja kumiliki laini zaidi ya moja ya mtandao mmoja hadi awe na kibali maalum, na sasa tunaona wimbi la watu kusajili laini ovyo kwa majina ya wengine na kwa vitambulisho feki vya taifa. Matukio haya yanalitia taifa doa kwamba zoezi la usajili wa laini kwa alama za vidole lilikuwa kiini macho, au ni sawa na usajili wa simu ili kuzuia simu za viwango hafifu kuingia nchini, ambazo zimejaa sokoni kwa sasa.


Kwa hali hii tunaweza kuhoji je, wizi mtandaoni hautibiki? Ni kikundi cha kina nani kisichogusika? Lini jambo hili litaisha na wahusika kukamatwa? Lini usajili wa laini utakuwa na maana ikiwa sasa ni holela? Leo hii mwananchi akipotelewa na laini yake kupata mpya ni utaratibu wenye usumbufu zaidi kuliko kusajili mpya. Ni muhimu sana suala hili likapewa kipaumbele na mamlaka zote zikahakikisha zinachukua hatua madhubuti kwa kufanya kazi kwa ushirikiano kwa maana ya polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Hali ikiachwa hivi, kwamba usajili kwa alama za video umekosa nguvu basi sasa haitashangaza kusikia kuna vitambulisho feki vya utaifa ambavyo vinatumika hadi kufungua akaunti kwenye baadhi ya benki, kiasi cha watu kuibiwa fedha za malipo mbalimbali kama pango la nyumba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tujipange kuzoa taka pamoja, kuzitupa ovyo huwa inakera

Na Yasmine Protace

**USAFI** ni msamiati unaoeleweka kwetu sote. Pia ni jambo linalofahamika vyema kwa wengi nyumbani, shule, hospitali kwenye mjumuiko na hata maisha binafsi.

Pale tunapozama kwenye kamusi inatajwa kwa tafsiri ya kidarasa kwamba "ni hali ya kutokuwa na uchafu.' Ikirejewa katika maisha ya mwanadamu, inabeba sifa kuu mbili, moja kuwa salama kiafya, pili mtu anakuwa katika wajihi wa kupendeza mtanashati au maridadi.

Ni jambo ambalo katika jumla yake, inazaa mazingira inayobeba tafsiri ya kuwajibisha kuwapo jukumu la kila mtu ajikite katika usafi na dhana hiyo inaanza kwa yule anayelifikiria hilo.

Pale usafi unapofanywa au kufanyika kwa namna yoyote ile, unasaidia kumlinda mtu dhidi ya baadhi ya magonjwa kumfikia mahali aliko, hata kupendezesha mazingira.

Katika sehemu za biashara, nako usafi unapofanywa unasaidia kuyaweka bora ya mafanikio katika nafasi na shughuli zinazofanyika.

Mkoani Dar es Salaam, kulikuwapo na utaratibu wa kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, hatua iliyoasisiwa na serikali inayotajwa imesaidia kwa kiasi kikubwa usafi wa jiji.

Pia suala la usafi lilikuwa linafanywa na mikoa mingine, likiasisiwa jijini Dar es Salaam, pale Hayati Rais John Pombe Magufuli alipoamua kushirikiana na majirani zake wa Ikulu, wafanyabiashara wa Feri, mwanzoni tu mwa uongozi wake.

Hapo ndipo ilipozaliwa kalenda hiyo ya usafi kitaifa. Kadri muda unavyoenda sasa, mambo yanabadilika. Hivi sasa mitaani Dar es Salaam, pamoja na kuwapo magari yanayochukua taka, bado kuna shida ya baadhi ya watu, wanaanza kuweka kando ustaarabu, wanaishia kuzitupa taka kiholela.

Kutoa taka kila wiki kuna gharama kote, kuanzia mtoaji hadi kwa halmashauri husika. Lakini, kinachoshangaza watu bado wanatupa taka hizo ovyo, ikiwamo mitaroni kunakopitisha maji machafu, hali inayosababisha izibe na kuzaa kero mpya.

> **Kutoa taka kila wiki kuna gharama kote, kuanzia mtoaji hadi kwa halmashauri husika. Lakini, kinachoshangaza watu bado wanatupa taka hizo ovyo, ikiwamo mitaroni kunakopitisha maji machafu, hali inayosababisha izibe na kuzaa kero mpya.**

Ukija upande mwingine, kuna wafanyabiashara katika maduka na vituo vya daladala vikubwa, unakuta uchafu umetapakaa mbele ya biashara zao, huku wahusika wakishindwa kutoa bila ya sababu ya kina.

Kwa kufanya hivyo, iko wazi kunazidi kuyafanya maeneo ya biashara na makazi kuwa machafu zaidi. Tumebahatika kwamba, sasa magari yapo na tunastahili kuyatumia kukidhi shida zetu, kwanini tunapuuzia?

Hapo tutaongea mengi, lakini kwa asilimia kubwa, hakuna sababu kuu inayoweza kutolewa utetezi wa kisayansi.

Ukishazungumzia usafi, anza na wewe mwenyewe uliko na kwa usafi wa jumla katika mazingira, anza na kile kinachotawala ndani ya mazingira yako, kulia, kushoto, mbele na nyuma yako.

Kama mtu atategemea hata taka zake kuzitupa kwa wenzake, ajue tayari anakaribisha magonjwa pasipo sababu za msingi kibinadamu na si mdau wa mazingira, bali mchafu.

Nasifu kanuni wanazotumia baadhi ya wazoa taka kutoa huduma kwa kuwavumilia wasio nacho siku hiyo, kisha kesho wanalipwa wakipita. Ushirikiano ni muhimu kwa jumla.

Ni suala linalotakiwa lifanyike katika mfumo wa pamoja na kamwe si kusimama pekee, kwani uzalishaji taka una kawaida ya kupatikana katika namna ya pamoja, vivyo hivyo inakabiliwa kwa kundi. Pamoja tutafanikiwa.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya akitoa tamko la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dar es Salaam jana, kwa kusimamia utawala wa sheria. Wengine ni viongozi wenzake, Gabriel Duwe (kulia) na Everist Majaliwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima sasa waiangukia serikali mgogoro na wafugaji

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

BAADHI ya wakulima katika Kata ya Mbwewe Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani, wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro kati yao na wafugaji ambao unaosababishwa na mifugo kuharibu mazao mara kwa mara.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, walisema wamekuwa wakiomba viongozi wa serikali wafike, lakini maombi yao hayajatekelezwa.

Mmoja wa wakulima hao, Hamis Rashid, ambaye alinusurika kuchomwa mkuki na mfugaji aliyekuwa akilisha mifugo karibu na shamba lake la mahindi, alisema kwa sasa hali si salama, na kwamba wanakoelekea kuna hatari ya kutoweka kwa amani kati yao na wafugaji.

"Leo nimenusurika kwa kuwa kuna watu wengi hapa, lakini ipo siku mtasikia mambo mengine, hakuna mtu anaweza kuendelea kuvumilia kupata hasara, analima haambulii kitu na hawa wafugaji wanaendelea kulisha mifugo yao kwenye mashamba yetu ...hii haikubaliki, viongozi wafike, vinginevyo wanataka amani itoweke," alisema.

Alisema mbali ya machafuko ambayo yanaweza kutokea, pia hofu ya njaa inatawala kwa wakulima, kwa kuwa mazao yanapoendelea kuharibiwa shambani hakuna mavuno yatakayopatikana.

Naye Christopher Magala alisema viongozi wanaohusika wanatakiwa kutathmini nafasi zao kwa kushindwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji katika eneo hilo, hivyo kusababisha mashamba kuendelea kuharibiwa.

Diwani wa Mbwewe, Omari Msonde, alisema migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa ikikua siku hadi siku, kutokana na wafugaji kulisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Msonde ameomba Mkuu wa Mkoa, Abubakar Kunenge, baadaye afike katika kata hiyo kufanya mkutano na wananchi kupata suluhisho la haraka, hivyo kurejesha hali ya amani.

Alisema yapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi hususani wakulima, ambao wamekuwa wakilishiwa mazao yao, huku wakishangaa kutokana na mashamba ya wafugaji ambayo mazao yamekua vizuri bila kupitishwa mifugo.


**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC**

## TANGAZO

### MKUTANO MKUU WA TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC (TACOBA)

TAARIFA INATOLEWA KWAMBA MKUTANO MKUU WA WANAHISA WA TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC AMBAYO PIA INAJULIKANA KAMA BENKI YA WANANCHI YA TANDAHIMBA (TACOBA) - UTAFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 19 JUNI 2021, KATIKA UKUMBI WA MAGHALA YA CHAMA CHA USHIRIKA TANDAHIMBA NA NEWALA (TANECU) – TANDAHIMBA MJINI KUANZIA SAA 3.00 KAMILI ASUBUHI.

- WANAHISA WOTE MNAKARIBISHWA KUFIKA KWA WAKATI MKIWA NA HATI ZA HISA AU STAKABADHI ZA UNUNUZI WA HISA.
- WANAHISA AU WAWAKILISHI WAO WATAJITEGEMEA KWA GHARAMA ZA USAFIRI NA KUJIKIMU.

**KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA KATIBU WA BENKI AU MENEJA MKUU WA BENKI YA TANDAHIMBA COMMUNITY BANK.**

**Tangazo hili limetolewa na;**
**KATIBU WA BENKI,**
**Tandahimba Community Bank Plc,**
**S. L. P. 06, Tandahimba, MTWARA**

**KWA IDHINI YA BODI**

**J. B. Rugambo**
**KATIBU**

**18 Mei 2021**


# Samia afagiliwa kufuta kesi zisizo na ushahidi

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusaidia kufutwa kwa kesi 147 zilizokuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) bila kuwa na ushahidi.

Aidha, imeitaka TAKUKURU iendelee kufanya hivyo, kama njia ya kusimamia utawala bora.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, alipokuwa akitoa tamko la CEGODETA na kumpongeza Rais kwa hatua hiyo na kuongeza kuwa anasimamia utawala wa sheria.

"Utawala bora hauruhusu kumhukumu mtu bila kumsikiliza, bali anatakiwa kupewa nafasi ili ijulikane kama ana kosa au la, Rais ameona mapungufu hayo kwamba yanakwenda kinyume na utawala bora," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya alisema, taasisi hiyo iko nyuma ya Rais, na kwamba itakuwa tayari kutoa ushauri kwenye mambo ya utawala bora pale itakapohitajika ili kusaidia kumaliza kero za watu kubambikiwa kesi.

"Tumemsikia Rais akisema kwenye vyombo vya habari kuwa kesi 147 zilizokuwa TAKUKURU bila ushahidi zimefutwa, hili ni jambo jema, lakini kumekuwapo na tuhuma zinazohusu baadhi ya polisi kuchukua bangi na kuwekea watu mifuko kwa lengo la kutaka wafungwe, huo si utawala bora," alisema.

# Makatibu Muhtasi 2,900 wanolewa Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKATIBU Muhtasi 2,900 kutoka Tanzania Bara na Visiwani wamekutana jijini Arusha kwa siku tatu, kwa ajili ya kujengewa uwezo na kuboresha utendaji wa kazi zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha, Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Muhtasi Tanzania (TAPSEA), Zuhura Maganga, alisema mkutano huo wa nane unafunguliwa leo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa. Zuhura alisema mkutano huo wa siku tatu una kaulimbiu "Kuwa mbunifu, mahiri, zingatia weledi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi Tanzania."

"Mkutano huu wa siku tatu unawashiriki zaidi ya 2,900 lengo likiwa ni kuwajengea uwezo na kubadilishana uzoefu na jinsi ya kutatua changamoto zinazowakabili," alisema," alisema. Alisema katika mkutano huo mada mbalimbali za kitaaluma zitatolewa ikiwamo utunzaji wa siri za ofisi, wajibu wa kila mtumishi katika eneo lake la kazi na kuongeza umahiri katika nyanja za utawala sehemu za kazi. Pia mada ya kupata ujuzi mpya na maarifa yanayoendana na sanyansi na teknolojia.

Awali Katibu wa chama hicho, Anneth Mapima, alisema tasnia hiyo imepiga hatua tofauti na awali, hivi sasa wanaweza kusoma hadi ngazi ya shahada ya kwanza.

# Vifo vya moto vyaongezeka

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

VIFO vinavyotokana na ajali za moto vimeongezeka nchini kutoka 33 mwaka 2018/19 hadi 123 mwaka 2019/20.

Akizungumza na waandishi wa habari Manispaa ya Morogoro katika maadhimisho ya wiki ya zimamoto na uokoaji kitaifa, Mkufunzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji, Rajabu Mwangalamo, alisema kuongezeka kwa vifo hivyo kumetokana na ajali ya moto iliyotokea mwaka 2020 Masnispaa ya Morogoro.

Mwangalamo alisema katika mwaka 2018/19 matukio ya moto yalikuwa ni 1,831, maokozi yalikuwa 593 na vifo 33 wakati katika mwaka 2019/20 matukio ya moto yalikuwa 1912, maokozi 952 na vifo 123.

Alisema kuongezeka kwa vifo hivyo pia kumesababishwa na kuongezeka kwa matukio ya kuungua shule mbalimbali zikiwamo za kiislamu kwenye mikoa mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mwangalamo, katika kipindi cha mwaka 2018/19, shule zipatazo 32 ziliungua, ambapo mwaka 2019/20 shule 33 ziliungua wakati shule moja mkoani Kagera jumla ya watoto 10 walipoteza maisha, nyingine mbili Dar es Salaam watoto 13 walipoteza maisha.

Alisema kuongezeka kwa matukio ya moto kunasababishwa na jamii kutosimamia vyema Sheria za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, na kwamba katika shule zilizopatwa na majanga ya moto, ilibainika kuwapo kwa uzembe na upuuzaji wa sheria hizo uliofanywa na wakuu wa shule.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Simon Karikari, akichangia mtazamo wake jinsi maendeleo ya teknolojia yanavyoweza kuongeza ufanisi wa biashara, wakati wa hafla ya Wiki ya Ubunifu, jijini Dar es Salaam juzi, ambapo Tigo ilikuwa mfadhili mwenza wa hafla hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndikilo apigania wafanyabiashara wasibomolewe

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amemwomba Mkuu mpya wa Mkoa huo, Abubakari Kunenge, kusimamia suala la bomoabomoa katika mji wa Mailimoja lisiendelee kwa kuwa linaweza kusababisha hasara na umaskini kwa wananchi.

Ndikilo alitoa rai hiyo jana katika hafla ya makabidhiano ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa, yaliyofanyika Kibaha na kuhudhuriwa na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, wenyeviti wa halmashauri, wakuu wa taasisi, watumishi na wadau wengine wa mkoa huo.

Alisema suala la bomoabomoa katika mji wa Mailimoja amelipigania kwa miaka saba, wananchi wasibomolewe mita 120 kwa kuwa wafanyabiashara wengi wa mji huo wamejenga maduka ambayo ndio yanawainua kiuchumi.

"Ndugu yangu Kunenge mji huu wa Mailimoja ilitakiwa kuvunjwa mita 120 ndani ya miaka saba nimepigania zisivunjwe hizo na palipobaki huenda Wakala wa Barabara wakawa wanahitaji kupavunja, saidia katika hili huu ndio mji mtu akifika hapa anatakiwa kujua yuko makao makuu ya mkoa, unatakiwa kutengenezwa na sio kuendelea kuvunjwa," aliomba Ndikilo.

Alisema, Kunenge anatakiwa kuwapigania wananchi wa Mailimoja waendelee kubaki katika eneo hilo, lakini paboreshwe na kutengeneza vizuri uonekane mji na kuondoa utata wa makao makuu ya Mkoa wa Pwani ambayo yapo Kibaha.

Akiongea baada ya makabidhiano hayo, Kunenge aliahidi kufanyia kazi yaliyoelezwa na Mhandisi Ndikilo. Aidha, Kunenge alisema katika hali ya maendeleo hazikosekani changamoto na kuwataka wataalamu kusimama katika nafasi zao za utendaji.

Alizitaka halmashauri kufanya kazi kwa bidii katika upande wa makusanyo kuhakikisha mapato ya yanaongezeka.

# Uhaba wa miundombinu shuleni waathiri wanafunzi wenye ulemavu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SHULE ya Msingi Buhangija jumuishi Manispaa ya Shinyanga, ambayo inafundisha wanafunzi wenye ulemavu, inakabiliwa na upungufu wa madarasa saba yenye miundombinu rafiki kwa wanafunzi hao.

Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Fatuma Jilala, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ilipotembelea shuleni hapo.

Alisema shule hiyo ina jumla ya madarasa 23, lakini yenye miundombinu rafiki dhidi ya wanafunzi wenye ulemavu ni 16, na kusalia madarasa saba, ambayo nayo yapo kwenye hatua ya ujenzi.

"Shule yetu tunafundisha wanafunzi wazima na wenye ulemavu mbalimbali, wakimo wasioona, kusikia na wenye ulemavu wa viungo... changamoto tulio nayo ni madarasa saba kutokuwa na miundombinu rafiki kwao," alisema Jilala.

Naye Ofisa Elimu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, alisema fedha za ujenzi wa miundombinu rafiki madarasa hayo saba zimeshatengwa Sh.milioni 15, na ujenzi wake utaanza hivi karibuni.

Mmoja wa wanafunzi wenye ulemavu Modesta Daudi anayesoma darasa la nne, alisema shule inapokosa miundombinu rafiki kwao, inawakwaza wakati wa kuingia darasani na hata kwenda msalani.

# Wahandisi wabanwa miradi ya kimkakati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wahandisi kuhakikisha wanakamilisha miradi yote mikubwa ya kimkakati iliyoanzishwa na serikali ya awamu tano kwa wakati ili kukuza uchumi na kufikia azma ya kujenga Tanzania ya viwanda.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia ujenzi, Mhandisi Joseph Malongo, alitoa maelekezo hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua warsha ya siku tatu kwa wahandisi.

Alitaja miradi hiyo ni daraja la Salenda, Daraja la Busisi, miradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere na reli ya kisasa.

"Serikali iliyopita iliandaa miradi mikubwa ya kimkakati na serikali ya awamu ya sita imeahidi kutekeleza... wahandisi mnajukumu kubwa la kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati kwa sababu kukamilika kwake itakuwa ni chachu ya maendeleo kwa Taifa," alisema.

Aliongeza: "Kwa nchi hizi ambazo bado zinaendelea sekta ya ujenzi ni muhimu sana kwa sababu inachangia asilimia kubwa ya maendeleo ya viwanda na biashara, hivyo kuongeza ukuaji wa uchumi."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wahandisi, Prof. Ninatubu Lema, alisema wamejipanga kuhakikisha wanashirikiana na serikali kukamilisha miradi yote mikubwa ambayo tayari ilishaanzishwa.

Alisema serikali imewapa jukumu hilo la utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo hivyo nao watajitahidi kuhakikisha wanakwenda kufanya kazi hizo kwa weledi mkubwa.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutuamini wahandisi, ndio maana tumeandaa warsha hii ili kujadili mambo mazuri ya uendeshaji miradi nasi tutaishauri serikali nini kifanyike ili tukamilishe miradi kwa wakati," alisema.

Naye Msajili wa Wahandisi, Mhandisi Patrick Barozi, alisema mafunzo hayo yataenda sambamba na kutafakari chanzo cha wahandisi wengi wa miradi ya maji kushindwa kutekeleza miradi hiyo kwa wakati na kusababisha kada hiyo kuongelewa vibaya na jamii.

"Kwa upande wa miradi ya maji malalamiko yamekuwa mengi hasa yakienda kwa wahandisi, sasa kwenye warsha hii tutajua kwanini malalamiko yanakuwa mengi na tatizo liko wapi na nini kifanyike ili kuondoa malalamiko hayo," alieleza.



Mafundi wakiandaa msingi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Nyabaengere, Kata ya Musanja, Musoma Vijijini, mkoani Mara juzi, ambayo inajengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao na wadau wengine wa afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lataka utafiti wa miradi h/shauri kabla ya utekelezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa imeshauri kufanyika utafiti wa kina kabla ya kutekelezwa miradi kwenye halmashauri ili iwe na tija. Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Abdallah Chaurembo, alitoa ushauri huo juzi wakati akihitimisha ziara ya kamati hiyo katika Soko la Ndugai jijini hapa. Alisema kwa sasa kumekuwa na wimbi la halmashauri kutaka kuendesha miradi ya soko lakini imeshindwa kuwa na ufanisi.

"Ni vyema utafiti wa kina ufanyike ili kuepuka kuweka fedha za umma kwenye miradi ambayo haina matokeo, tunasoko la Machinga Complex limetumia fedha nyingi na hakuna kitu, kule Temeke kunasoko limejengwa halifanyi vizuri na pia wanataka kujenga lingine, hili lifike mwisho," alisema.

Awali, wakichangia kwa nyakati tofauti wabunge walishauri serikali kudhibiti madalali katika upatikanaji wa vizimba na ushushaji wa mizigo katika soko la kisasa la Ndugai.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema kushindwa kuimarika kwa biashara kwenye soko hilo kunatokana na madalali kuhodhi vizimba sambamba na kuzuia magari ya mizigo kushusha hapo.

"Madalali ni kikwazo kikubwa pale, unaweza kuta wamelipia vizimba na wakisubiri biashara ichanganye, hata yale malori tukiyokuta wakishusha mzigo tumekuta pale kwasababu Kamati ya Bunge imetembelea, ndio maana baada ya muda hakuna hata mkungu mmoja, imeenda wapi," alisema.

Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Constantine Kanyasu, alipinga wazo la kutaka kuhamisha Soko la Sabasaba na kushauri kuwa ni vyema kuwaondoa wale waliozidi na kufanya biashara zao barabarani na chini ndio wapewe vizimba kwenye soko la Ndugai.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka, alipinga uamuzi wa uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma ya kutaka kuhamishia sokoni hapo wauza mbao na gereji za katikati ya jiji kwa lengo la kuhamasisha biashara katika soko hilo.

Mbunge wa Ulyankulu (CCM), Rehema Migilla, alishauri uongozi wa Halmashauri ya Jiji hilo kutumia chombo cha tija kilicho chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuifanyia tathmini mradi huo wa soko la Ndugai.

Akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema walishabaini kero ya madalali na kuwa wameamua kutoa siku 14 kwa wale wote waliolipia kuanzisha biashara na kinyume chake watanyang'anya.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, aliwahakikishia wabunge kuwa watafanya mapitio ya mpango wa biashara wa soko la Ndugai ili uendane na kile kilichokusudiwa.

"Mradi wa soko la Ndugai ulibuniwa kwa kuangalia 'long time plan' kwa kuwa Dodoma imekuwa ni Makao Makuu ya Nchi, lakini ongezeko la watu, hivyo ni kweli zimewekwa Sh. bilioni 14.6, lakini ukiangalia makisio ya marejesho kiasi hicho cha fedha kitarudi," alisema. Meneja wa Soko la Ndugai, Stephen Maufi, alisema mpaka sasa vizimba 318 kati ya 366 vimepata wateja, huku maduka 161 kati ya 175 pia yamechukukiwa na mabucha 7 kati ya tisa yameshapata wapangaji na mgahawa mmoja umepata mpangaji na mmoja bado haujapata.

# Dk. Mwinyi aipongeza China kuisapoti Zanzibar kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Watu wa China imepongezwa kwa kuendeleza utamaduni wake wa kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta za maendeleo ikiwamo mikakati iliyowekwa katika kuimarisha uchumi wa buluu.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alitoa pongezi hizo Ikulu mjini Zanzibar wakati alipofanya mazungumzo na Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China, Zhang Zhisheng, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha.

Rais Dk. Mwinyi alieleza kuwa Jamhuri ya Watu wa China ni mdau muhimu wa maendeleo ya Zanzibar, kwani imekuwa ikiiunga mkono Zanzibar tokea miaka ya 60 baada ya Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964.

Alimweleza Balozi huyo mdogo wa China anayefanya kazi zake Zanzibar kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamani sana juhudi za Serikali ya China katika kuunga mkono miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alisema Jamhuri ya Watu wa China imeweza kuunga mkono sekta mbalimbali za maendeleo hapa Zanzibar ikiwamo afya, elimu, kilimo, viwanda na nyenginezo.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alieleza kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar ina furahishwa na juhudi za nchi hiyo za kuendeleza uhusiano na ushirikiano wake katika kuendeleza na kuimarisha sekta za maendeleo.

Mapema Balozi mdogo wa China Zhang Zhisheng alimweleza Dk. Mwinyi kuwa Jamhuri ya Watu wa China inathamini uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na kuahidi kuendeleza kwa manufaa ya pande zote mbili.

Alimweleza Rais Dk. Mwinyi kuwa Jamhuri ya Watu wa China iko tayari kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uchumi wake kupitia dira ya uchumi wa buluu pamoja na kulipokea wazo la kuwakaribisha wawekezaji kutoka nchini humo.

# TASAC yahudumia meli za nje 439 kwa miezi 14

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limesema tangu Februari mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, limehudumia meli 439 zilizowasili nchini na kwamba hivi sasa kuna ongezeko la mahitaji ya huduma linalokua kwa asilimia 8.3.

Limesema, hali hiyo inafanya baadhi ya shehena kuchelewa kupakuliwa na kuondoshwa kwa mizigo bandarini, kutokana na wingi wa meli zinazowasili nchini, pamoja na uwezo wa gati katika Bandari Kuu ya Dar es Salaam.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Meli kutoka TASAC, Nelson Mlali, aliyasema hayo jana kwenye semina ya kuwajengea uwezo wanahabari kuhusu shughuli za majini, iliyofanyika mkoani humo.

Alisema tatizo la shehena zenye bidhaa na mizigo mbalimbali zilizowasili kutoka nje ya nchi, kuchelewa kuwafikia wateja, kiasi kikubwa hutokana na ongezeko la meli na kukua kwa biashara huku kwa mwezi wakihudumia takribani meli 37.

"Shirika hili kwa asilimia 8.3 linakuza biashara na hutoa huduma kwa asilimia 30 ya meli zote zinazowasili nchini, huku iliyobaki, zinahudumiwa na mawakala binafsi," alisema Mlali.

"Gati za kupakua shehena zenye mizigo na bidhaa tofauti hutofautiana, kwamba ni bidhaa ya chakula zina gari yake, kadhalika zisizooza au zinazooza. Kipaumbele huwa kwa aina ya mzigo, ikiwamo chakula, pengine hata kuna dharura.

"Kadri huduma inavyokwenda haraka kupakua, kupakua shehena ndivyo mapato yanavyoongezeka, tunashirikiana na wadau ili kuharakisha huduma," alisema Mlali.

Aliongeza, umakini unahitajika katika kutunza nyaraka za mizigo na kwamba upotevu wake huwa hasara na kupoteza mapato kwa nchi na kwamba shirika hubeba dhamana ya afya ya mabaharia na wahudumu waliowasili na meli, ikiwamo kutoa huduma za tiba kwa dharura.

Ofisa kutoka Kitengo cha Uhakiki wa Mizigo Inayoingia, TASAC, Jenifer Matemba alisema uhakiki wa awali wa nyaraka zilizowasilishwa kabla ya meli kuwasili, husaidia kufanya maandalizi ya mapokezi ya meli kufanya ukokotoaji wa ushuru sahihi, kuandaa vifaa vya upakuaji kulingana na aina ya mizigo inayowasili.

"Mzigo unapowasili tunaoanisha na nyaraka zilizowasilishwa awali, kubaini vinaendana na kuanza kupakua," alisema Matemba.




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro (katikati) akipokea baadhi ya nakala 2,000 za vitabu vya mwongozo wa kuzuia na kufichua uhalifu katika kata/shehia kutoka kwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Jamii wa Kampuni ya vinywaji ya Coca Cola, Salum Nassoro, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# UDSM yajivunia utafiti dawa ya corona

**Na Enock Charles**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam kimesema mojawapo ya kazi za kiutafiti za hivi karibuni inayojivunia ni suala la utafiti kuhusiana na dawa ya Udanol Fukiza ambayo kimesema imesaidia kupunguza makali ya virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kuwakaribisha wadau mbalimbali katika maadhimisho ya sita ya wiki ya utafiti na ubunifu chuoni hapo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha Utafiti, Prof. Bernadeta Killian, alisema baada ya kuona uhitaji wa dawa hiyo umekuwa mkubwa kutokana na matokeo yake kwa walioitumia, waliamua kupanua maabara ili kuzalisha kwa wingi.

"Kwa sasa hivi lengo letu ni kutoa fedha zaidi kwa hii timu ya utafiti kwa sababu wamegundua kwamba watu wamekuwa wanatumia hii dawa ya fukiza mara nyingi tukiihusisha na corona, lakini kuna wengine wametoa taarifa ya kupona magonjwa mengine ," alisema Prof. Kilian.

"Kuna mwingine alikuwa ana baka ambalo haliponi kichwani, akaamua kupaka imefuta, mwingine koo lilikuwa linampa tabu kwa miaka mingi ametumia dawa hii ameponywa ile imeisha." Aliongeza.

Aidha, chuo hicho kimesema kwa sasa kimeingia katika makubaliano na Halmashauri ya Geita ili kutengeneza gari ambalo litatumia betri ya umeme ambalo halitatumia mafuta na kuepuka uchafuzi wa mazingira, kufikia Septemba mwaka huu gari hilo liwe barabarani.

## TADB, Chuo cha Utalii wanufaisha wanawake

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa kushirikiana na Chuo cha Utalii cha Taifa (NCT) wanaendesha mafunzo ya siku tatu kwa wanawake wajasiriamali wanaojihusisha na kutayarisha, kuchakata na kusindika chakula cha asili ili kuwaongezea uwezo pamoja na thamani ya bidhaa zao.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na Chuo cha Taifa cha Utalii Makao Makuu jijini Dar es Salaam pamoja na matawi yake yaliyopo Arusha na Mwanza ambapo jumla ya shilingi milioni 15 zimetolewa na TADB ili kuwezesha mafunzo kwa wanawake 150.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Wanawake wa Wilaya ya Temeke, Herieth Makombe, ambaye alimwakilishi Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, alisema mbali ya kuipongeza TADB kwa juhudi zake za kuwezesha wakulima na kuwaunganisha kwenye mnyororo wa thamani, amewataka wanawake hao kutumia vyema mafunzo watakayoyapata.

"Tumieni nafasi mliyoipata katika kujiimarisha na kujiongezea uwezo wenu katika kutayarisha, kuchakata pamoja na kusindika vyakula vya asili ambavyo vimekuwa kiungo muhimu katika kutangaza utamaduni wa Mtanzania. Tunaamini jitihada hizi za TADB na Chuo cha Utalii zitawaongezea fursa kubwa kwenye soko la ndani na nje ya nchi," alisema Herieth.

Ofisa Mwandamizi wa TADB anashughulikia kitengo cha Wanawake, Vijana, Chakula na Lishe, Mboka Mwanitu, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Benki, Japhet Justine, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha uwezo wa wanawake katika tasnia ya utoaji wa huduma ya chakula.

## Tume: Tanzania ina miundombinu imara

**Na Beatrice Moses**

TUME ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) imesema Tanzania ina miundombinu imara ya TEHAMA inayowawezesha Watanzania kujenga uchumi wa digitali na imeahidi kuwajengea uwezo Watanzania watakaojitokeza juu ya matumizi ya digitali ili kuongeza tija katika uchumi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kufuatia mkutano wa mabingwa wa TEHAMA wa hivi karibuni, Katimu Mkurugenzi wa Tume ya TEHAMA, Mhandisi Samson Mwela , alisema kwa sasa duniani kote uchumi unaendeshwa na mifumo ya TEHAMA na kueleza kwamba lazima uchumi waTanzania uendeshwe kwa mifumo ya TEHAMA maana Tanzania siyo kisiwa kilichopekee duniani.

Ameahidi kuwa tume itashiriki kikamilifu katika kujenga raslimaliwatu ili kupata wataalamu wa kutumia rasilimali za TEHAMA zilizopo ili kujenga uchumi.




Ukurasa 13

Tuendelee kukatakata mikoa kweli?

BUFE
IJUMAA MEI 21, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 12



**SUA- TAWI MIZENGO PINDA Nuru mpya utalii, ufugaji nyuki na kilimo Nyanda za Juu Kusini**

# DK. KALEMANI ALIPOJINASIBU MANYARA REA IMEFIKISHA UMEME KILA UPENYO

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

WAKATI kuna Watanzania wengi wanafurahia nishati umeme inayotolewa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), je ni wangapi wamejiuliza, ufadhili wake ukoje?

Dk. Medard Kalemani, waziri mwenye dhamana alitengua kitendawili hicho Aprili 24 mwaka huu mkoani hapa, alipoambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), inayoongozwa na Mwenyekiti Naghenjwa Kaboyoka.

Anasema mapato ya REA, yanatokana na tozo kwa wazalishaji umeme binafsi, wamiliki wa vyombo vya usafiri na watumiaji mafuta ya taa; kila lita moja ya petroli na dizeli anayoweka mteja REA inakatwa fedha.

Pia, kuna asilimia 10 kutoka wadau wa maendeleo kimataifa nchi kama Sweden na Norway na anaeleza Dk. Kalemani: "Hizi ni fedha za walipa kodi kutoka kwa watumiaji kama una kibatari tunakukata Sh. 150 ingawa vibatari vimepungua,"



Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo (Kushoto), akifuatiwa na Waziri wa Nishati Dk.Medard Kalemani wakiwakaribisha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), inayongozwa na Mwenyekiti, Naghenjwa Kaboyoka (kulia). **PICHA: JALIWASON JASSON.**

**UMEME MANYARA**

Dk. Kalemani anasema kati ya vijiji 417 vya Manyara, 259 vimeishawekewa umeme na vilivyobaki 158, nako anaahidi kuvimalizia haraka, muda mfupi ujao.

Anasema serikali inadhamiria kufikisha umeme vijiji hadi kufika Desemba mwaka ujao. Nchi nzima, kuna jumla ya vijiji 1,956 vimeshapelekewa umeme.

Dk. Kalemani anaiambia Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, anasema Tanzania inaongoza kufikisha umeme kwa asilimia 85.

Kuhusu wateja wapya Manyara, Dk. Kalemani anasema, walitarajia kuwaunganishia umeme wateja 4000 na hadi mwezi uliopita, walishawaunganishia zaidi wateja wapya 800

"Taasisi za umma tutazipatia kipaumbele ziwe mbali au karibu kwa kipindi hiki tunachoendea kutekeleza mradi huu," anasisitiza

Waziri anasema, wakati mradi REA unaanza watu wengi walitumia mafuta ya taa na ndio maana wakaamua kuyatoza kuchangia REA.

Dk. Kalemani anasema, sasa kuna mabadiliko makubwa ambayo ni kiashiria umeme wa REA kusambaa, kwani mafuta ya taa yanayoingia nchini kwa mwezi ni lita milioni sita, lakini yanayotumika ni lita 600,000, asilimia 90 yanabaki.

Anasema, wameanza utaratibu wa kuweka nguzo za zege katika maeneo yenye maji au majaruba na anatoa mfano wa ugumu wa kazi, kwamba katika Wilaya ya Simanjiro hufika hatua kumpelekea mteja mmoja hugarimu hata nguzo 20, kwa sababu makazi ya jamii hiyo wafugaji wametawanyika.

"Serikali inalipia nguzo kwa asilimia 100 na TANESCO sasa haiendeshwi kwa hasara inajiendesha yenyewe," anajigamba waziri.

Alipokuwa kijijini Arri, aliwaahidi wananchi kwamba vijiji vilivyobaki 22 wilayani Babati, vingemaliziwa kuwaunganishia umeme baada wiki moja.

Waziri anatumia fursa hiyo kuwataka waanzishe miradi inayotumia umeme kama vile mashine za kusaga nafaka, ili wajiongezee kipato kwa kuwa wao ni wakulima bora.

Vilevile, anawataka wasihujumu miundombonu, naye akiwawahakikishia "umeme haubagui nyumba," hivyo zote zitafikishiwa. Anafafanua:"Bei hazibadiriki iwe ni ghorofa, tembe, nyumba ya misumari tu bei ni Sh. 27,000 tu."

Anaongeza kwamba umeme unapaswa kuingizwa kwenye mazizi ya mifugo kuimarisha ulinzi, akitoa mfano hatari za fisi wavamizi wa kwa mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**WABUNGE & WANAKIJIJI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Kaboyoka, anawahakikishia wanakijiji Arri, wataletewa umeme, kwani wao ni jicho la Bunge.

Anasema, ni haki kodi zao zifanye kazi inayoonekana, huku anawasifia TANESCO kwa kazi nzuri kushirikiana na REA.

Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, anasema asilimia 82 ya vijiji vyake vina umeme, akiamini vilivyobaki navyo vitapatiwa.

Mkazi wa Kijiji cha Nakwa, Bakari Juma, anaishukuru serikali kuwaona wanyonge kwa kuwasogezea umeme, akitaja ni mapinduzi makubwa yanayowaachia wananchi gumzo kubwa.

Mkazi wa Mtaa wa Mluki, Anna Samweli, anasema walizoea kwamba wanaounganishiwa umeme ni matajiri, lakini serikali imeondoa dhana hiyo kuwa ya wote.

Mkazi wa Sinai, Beatrice Chacha, anaishukuru serikali kuanzisha mradi uliowagusa wengi na anaiomba iwe endelevu kwa wengi zaidi wanufaike, akigusa shukrani kwa Hayati Rais John Magufuli.

Anasimulia, rais huyo wa zamani alipofika Babati alitoa maelekezo ya watu walioomba kuunganishiwa umeme watekelezewe haraka na imezaa neema kubwa kwa wengi walioishi nje ya mji.

Mwanamama huyo ana rai kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kuimarisha mradi REA uendelee kuwanufaisha wengi pasipo kujali tofauti zao za hali.

UCHUMI

# SUA- TAWI MIZENGO PINDA

# Nuru mpya utalii, ufugaji nyuki

## •Shambani mazoea basi, mapya Hifadhi Katavi

**Na Eliud Ngondo, Mbeya**

TANGU Uhuru wa nchi mwaka 1961 kilimo kimedumu kuwa nguzo kuu ya chakula na uchumi, hivyo kupewa wasifu uti wa mgongo wa taifa, tafsiri inayofika hadi nje ya mipaka.

Kilimo nchini kinaongoza kutoa ajira kwa wakazi zaidi ya theluthi tatu nchini, ndiye mlishaji mkuu wa Watanzania.

Ni sababu inayoifanya serikali kuwekeza kwa kina katika kwenye sekta hiyo, ikianzia na utoaji elimu na teknolojia ya kilimo bora kwa wananchi wake, ili kuifikia tija.

**SAFARI YA SUA**

Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), kiliasisiwa mwaka 1984, wakati huo kikiitwa Chuo Kikuu cha Morogoro na kilikuwa tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chimbuko la hoja lilikuwa kuandaa wataalamu wa kilimo wenye elimu ya juu, kukidhi mahitaji ya wakulima na wadau wa kilimo nchini.

Baadaye ilibadilishwa na kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine, hatua zilizoendana na ngazi ya kujitegemea kama ilivyo sasa

Jina la Sokoine, lilitokana na uhalisi kwamba aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Sokoine, alikiwa mpenzi na mfuatiliaji mkubwa wa kilimo.

Kimsingi, mahitaji ya wataalamu kilimo yamekuwa yakiongezeka nchini kila mwaka, kutokana na kuongezeko watu na teknolojia kukuai duniani.

Ili kuendana na kasi hiyo, SUA ilianzisha Ndaki (Constituent College) ya Mizengo Pinda, baada ya kukabidhiwa majengo yaliyopo katika kijiji cha Kibaoni, katika Halmashauri ya Mpimbwe wilayani Mlele, mkoani Katavi.

Mgeni rasmi kwenye ufunguzi alikuwa mpenzi wa kilimo, Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda. Serikali imeanzisha malengo maalum ya kutoa mafunzo, ikiwamo Diploma ya Usimamizi wa Kilimo na Uzalishaji, pia Kuongoza Watalii na Uwindaji Bora.

Mafunzo mengine ni ya ngazi ya cheti katika fani ya Kusimamia Watalii na Shuguli za Uwindaji, pia shahada ikiwamo ya kusimamia nyuki.

**MWENYEKITI BODI**

Mwenyekiti wa Bodi ya Ndaki ya Mizengo Pinda, Dk. Tulole Bucheyeki, anasema chuo kimeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha kinazalisha wataalamu wengi na teknolojia bora za kilimo, ufugaji nyuki na utalii.




Viongozi wa kiserikali na wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Ndaki ya Mizengo katika picha ya pamoja.

> **“Pia, ukumbuke kuwa palipo na misitu mingi hasa ya asili lazima nyuki wanapatikana, hivyo basi mikoa hii ya Katavi, Rukwa, Tabora na Mbeya imekuwa ikizalisha asali kwa wingi na kusababisha uwapo wa hitaji la kupata wataalamu wa fani ya ufugaji nyuki” anasema Dk. Bucheyeki.**

Dk. Tulole ambaye pia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, anasema serikali imekusudia ndaki hiyo kuwa kitovu cha uzalishaji wataalamu wa teknolojia bora za kilimo zitakazotumiwa na umma.

Katika hilo, wakazi wa Nyanda za Juu Kusini ndio walengwa wakuu wa kuletewa tija shambani na uzalishaji chakula.

Dk. Bucheyeki anasema wao kuwa na mitaala ya ufugaji nyuki, kilimo na utalii ina malengo maalum ya kuinua sekta za utalii na ufugaji nyuki katika ukanda huo jirani.

“Kijiografia Ndaki hii ya Mizengo Pinda ipo jirani kabisa na Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Serikali imeona inaweza kutumia ndaki hii kuzalisha wataalamu wengi wa fani ya kuongoza watalii, lengo likiwa kuinua sekta ya utalii kwenye mikoa hii na hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

“Pia, ukumbuke kuwa palipo na misitu mingi hasa ya asili lazima nyuki wanapatikana, hivyo basi mikoa hii ya Katavi, Rukwa, Tabora na Mbeya imekuwa ikizalisha asali kwa wingi na kusababisha uwapo wa hitaji la kupata wataalamu wa fani ya ufugaji nyuki” anasema Dk. Bucheyeki.

Anaahidi katika kipindi chake cha uongozi, kwamba Ndaki ya Mizengo Pinda itakuwa kitovu cha teknolojia za kilimo, ufugaji bora nyuki na mazingira, pia chachu ya kukuza teknolojia kwa umma jirani, anaoamini wataunga mkono zawadi hiyo ya kiserikali.

**KINACHOFANYIKA**

Mkuu wa Ndaki ya Mizengo Pinda, Prof. George Mwamengele, anafafanua kwamba kupitia tafiti mbalimbali za wahadhiri na wanafunzi, zitasaidia kubaini shida za wakazi na ufumbuzi wake.

Prof. Mwamengele, pia anadokeza imani yake Hifadhi ya Taifa ya Katavi, itakiwa manufaa ya moja kwa moja, kutokana na ujirani wao.

Makamu Mkuu wa Ndaki ya Mizengo Pinda, Prof. Anna Sikira, anasena kutafanyika tafiti shirikishi zitakazowawezesha wataalamu wa chuo kuelewa kwa undani mazingira na jamii jirani, hata wakatambua magumu yao.

Prof. Anna anasema, chuo kina utaratibu wa kuzunguka katika shule za sekondari jirani hasa zenye madarasa ya kidato cha sita, kuwahamasisha vijana kusoma kwa bidii wafaulu kupata sifa ya kujiunga na chuo hicho.

Hapo analalamika kuwapo idadi ndogo ya wanawake wenzake, wanafunzi wa kike. Sasa wito wake vijana wa kike wanajitoleza zaidi kujiunga na chuo na kwamba kozi zinazotolewa chuoni humo zinaendana na fursa zilizoko katika mikoa jirani.

Prof. Anna, anatoa mfano wa kozi za; Kuongoza Watalii; Uwindaji Bora, Ufugaji Nyuki, na Utunzaji wa Mazingira zinazotolewa chuoni hapo, ambako ni umbali takriban kilomita 10 kutoka hifadhini, akizisifu zina manufaa makubwa kwa mikoa hiyo jirani iliyozingirwa na misitu.

Anasema, ndaki hiyo imeshaandaa mizinga mingi na kuitundika msituni kwa ajili ya kufundishia wanafunzi kwa vitendo. Pia, itakuwa kivutio cha wafuga nyuki jirani na chuo kujifunza.

Prof. Anna anataja mpango mkakati wao ni kwamba wanafunzi watakapopata elimu hiyo, utakuwa mtaji mkubwa kuwaambukiza majirani na ndio unakuwa mwanzo wa kuachana na kilimo cha mazoea.

Kwa mujibu wa Makamu Mkuu wa Chuo, hadi sasa wameshaanzisha shamba la kufundshia kwa vitendo na mfano bora wa kilimo cha kisasa na tafsiri kuu inalenga kufikia Nyanda za Juu Kusini, ambako anasema wananchi wanaifundishika.

**PAGUMU WAPI?**

Prof. Anna anasema bado wanafunzi wanaosoma chuo hicho, idadi kubwa ni wanaotoka mbali na kilipo chuo, akitoa ya wadahiliwa katika Shahada ya Ufugaji Nyuki hakuna anayetoka jirani.

Ni jambo linalomfanya mwanazuoni huyo kufanya kazi ya kuwashawishi walioko jirani kusoma kwa bidii wapate sifa za kujiunga.

Anataja kikwazo kingine, ni uchanga wa chuo ambacho hadi sasa kina mwaka mmoja, hakijajitangaza vya kutosha hata kupata wanafunzi wengi wa kujiunga nacho.

**WANAFUNZI WAFURAHIA**

Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Noel Mboya, anayesoma Shahada ya Uzalishaji Nyuki na Mazao Yatokanayo na Nyuki (Bachelor of Science in Bee Resource Management), anasema ufugaji bora wa nyuki ni njia kuu ya utunzaji mazingira, hivyo, anatarajia kutuimia elimu atakayoipata, kuyainua kwa umma, hasa utunzaji mazingira.

Anaeleza, pia ni hatua inayoendana na kulinda wa uoto wa asili unaoharibiwa kila siku, hata kufikia hatua kuwa tishio kitaifa.

Silas Manyara anayesomea Diploma ya Kilimo, anasema elimu wanayoipata inalenga kuwaumba wasaidizi wa taifa katika sekta mbalimbali za kilimo, ambacho ndicho tegemeo la nchi.

Akizungumza katika lugha ya kitaalamu, Manyara analalamika wakulima wengi nchini bado wako katika kilimo cha mazoea, hivyo ananuia kuleta mabadiliko yenye manufaa kiuchumi.


“Elimu ya kilimo tunayoipata itasaidia hata namna ya kutunza mazao yao kabla na baada ya kuvuna na kuyaongeza thamani ili yakipelekwa sokoni yaweze kuwa na tija zaidi,” anasema Manyara.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, katika mandhari ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Ndaki ya Mizengo, mkoani Katavi. **PICHA ZOTE: SUA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tuendelee kukatakata mikoa kweli?






**NA JOSEPH KULANGWA**

JIWEKEE utaratibu wa kila ukisikia mikutano ya kiongozi wa juu kitaifa amefika kijijini kwako, au hata katika kijiji kingine jirani au cha wilaya au mkoa mwingine, hudhuria.

Hutakosa kusikia matatizo mbalimbali ya kijamii, yakiwamo ya elimu, afya na maji. Orodha itakuwa ndefu na ikiwezekana watasimama jasiri na kuwashitaki viongozi wao kuwa walishasema, lakini hakuna kinachofanyika.

Kiongozi atasikiliza na pengine atawasimamisha viongozi kujieleza, na baada ya hapo atatangaza kuchukua hatua za kukabiliana na matatizo yanayowakabili wananchi na ikiwezekana hata muda wa kuyatatua atawapa.

Kwingineko, kama hakuna matatizo kama hayo, utasikia wanamwambia mheshimiwa kuwa mkoa huu ni mkubwa sana, tunaomba ugawanywe iwe miwili, ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

Nilishasikia hoja mikoa kama miwili hivi igawanywe. Pia, nasikia kuna vigezo kwa mkoa kugawanywa, au wilaya kuwa mkoa. Naambiwa ni idadi ya watu na uchumi. Utashangaa kimkoa ‘kidoonyo’ nacho kinalilia kugawanywa, kuwa mikoa mwili.

Hapo ina maana apatikane tena mkuu mwingine wa mkoa. Wilaya iwe mkoa, ili apatikane mkuu wa mkoa na wilaya zizaliwe kuwa na wakuu wa wilaya.

Isisahaulike kwamba wakuu wa mikoa wanakuwa na watendaji wao huku pia wakuu wa wilaya nao wakiwa na wa kwao. Hapo hata asiyebaini atamudu kujua, kuna ongezeko la matumizi ya umma.

Mishahara, marupurupu na mambo mengine yakiwamo ya usafiri, makazi matibabu na kadhalika.

Unajiuliza, hivi tunatafuta nini sisi wenue uchumi mdogo? Mbona Taifa kubwa kama Marekani, tangu lizaliwe takriban miaka 300 iliyopita, limekuwa na majimbo 50 tangu enzi na enzi, hatujasikia sasa jimbo hili ligawanywe, lizaliwe jimbo lingine?

Hapa kwetu mara zote kihistoria Baraza la Mawaziri linaelea katika hesabu ya wastani 20 na zaidi, ilhali Marekani taifa tajiri kwenye majimbo 50, lina mawaziri 15 tu tangu lizaliwe.

Na mawaziri hao wa kwetu, pia wizara zao ni zilezile, wala hazibadiliki sana. Hapa kwetu unasoma jina pana la wizara, kama si mweledi wa kusoma unaweza kukwama njiani, upana wa jina unadokeza kila eneo linalohusika nalo.

Binafsi nao si sahihi, jina hilo lingeweza kurekebishwa na kudokeza eneo mojawapo kuwakilisha kwa upana, mathalan Wizara ya Afya.

Nirudi kwenye mada yangu sasa, pia nadhani katika muundo wa wizara, haitakuwa jambo baya kupunguza idadi kwa kadri tutakavyoweza.

Inaweza kuwa hatua inayopaswa kuendana na udhibiti wa idadi ya majimbo ya uchaguzi, jimbo ligawanywe pale tu inapobidi sana, maana yote katika tafsiri pana ni gharama kwa umma wa walipa kodi nchini.

Majimbo mengi yana sura nyingine, kwamba ni ongezeko la idadi ya wabunge wanaopokea ‘njuluku’ chekwa, ambazo zingeweza kufanya mengine kwa masikini wenye kuhitaji na hata wako wasio na nyuma wala mbele.

Kuna watu huko nyuma waliwahi kuja na mapendekezo ya Tanzania kuwa na majimbo kama zilivyo nchi zingine za Afrika kama Nigeria na Afrika Kusini, ili kupunguza idadi ya viongozi wanaolipwa sana.

Lakini, hiyo ikapingwa vikali. Laiti wangesikilizwa, pengine ingesaidia kuachwa kukatakata nchi vipande. Si ajabu kuona wapo wanaoshikilia upande wa hoja kukatwa vipande, kwa sababu tu wanaona huenda kutapatikana uteuzi unaowagusa.

Hivi kweli mkoa mdogo unapogawanywa utakuwa na tija gani, zaidi ya kupunguza maeneo na kuongeza idadi ya wakubwa wanaolipwa vizuri?

Ni busara tukakuna ubingo katika hili kabla ya kufanyia uamuzi, ili kuona kama kinachozalishwa kina tija na fursa ya maendeleo au la. Tuige hata wenzetu basi. Alamsiki!

UCHUMI

# Mkurugenzi Jiji Dar afunguka siri Hati Safi, anavyojipanga aendako

- Akiri kilichotokea Jiji Dodoma kiliwagusa
- Kuna hospitali mpya, shule wasichana yaja
- Ajira walimu sekondari wa sayansi pekee



Mandhari ya Hospitali ya Kivule. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

MARA zote inaelezwa usimamizi bora wa mapato na vigezo vyake kihasibu mara zote inachangia katika mafanikio ya malengo katika eneo au taasisi husika, iwe ya umma au binafsi.

Pale mapato yasiposimamiwa vyema, maana yake ni kuweka mkondo wa kukosekana maendeleo.

Wakaguzi wa hesabu wana vigezo vya utoaji hati zao, ikianzia na Hati Safi; Isiyoridhisha; na Chafu. Pale inapopatikana Hati Safi ya Hesabu, inabeba maana ya vigezo vyote vya matumizi ya fedha na usimamizi wa huduma vimezingatiwa.

Hivi karibuni imekuwapo wimbo mkubwa wa kutafsiri mwenendo wa utendaji serikalini na hata kuwatia baadhi ya watendaji katika tuhuma nzito za jinai dhidi ya mali ya umma.

Kwa halmashauri mbalimbali zilizotapakaa sehemu mbalimbali nchini, baadhi zimefanikiwa kupata hati hiyo safi, ikipigiwa makofi ya kusimamia vizuri vyanzo vya mapato na mali ya umma, pia huduma na zipo zilizoporomoka kwa hati chafu na kuangukia majanga.

**JIJI DAR?**

Hivi karibuni Halmashauri ya Jiji la Ilala (ambalo sasa ni Dar es Salaam), lilitunukiwa Hati Safi, kutokana na kukusanya na kutumia vyema mapato yake vizuri.

Mkurugenzi wake, Jumanne Shauri, anaiambia Nipashe kwamba, siri ya kupatikana hati hiyo safi inatokana na kufanya kazi kwa ushirikiano, ikiwamo kusimamia mianya ya mapato na kuidhibiti inavyopaswa.

"Nashirikiana na wenzangu kudhibiti mianya ya mapato kwa kukisimamia na kuongeza mapato," anasema.

Mkurugenzi Shauri anasema, pale wenzao mkoani Dodoma walipopatiwa Hati Safi za ukaguzi, iliwapa hamasa kubwa na ndipo mwaka juzi wakati huo wakiwa Manispaa ya Ilala, walijipanga timu nzima kuhakikisha wanaipata Hati Safi.

Anadokeza swali walilojiuliza, ni kwamba inawezekanaje kushindwa kupata Hati Safi wakati wana mengi ya kuwaingizia mapato, ikiwamo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na mengine ya thamani zinazofanana nayo?

Anarejea uamuzi wa Hayati Rais John Pombe Magufuli kuitangza Manispaa Ilala kuwa jiji haikukosewa, kwani walikuwa na vigezo stahiki.

Anasema katika kipindi cha mwaka 2018 walikusanya fedha kiasi cha Sh. bilioni 44 na kwa sasa wamefikisha Sh. bilioni 60, wakiwa na malengo ifikapo mwaka 2025 wakusanye Sh. bilioni 100.

Anasema namna wanatumia pesa zao kwa kiasi kikubwa wanazielekezea katika miradi mikubwa ya maendeleo, wakati huohuo wanakumbuka vyema wajibu wao wa kila halmashauri inatakiwa kutenga fedha asilimia 10 ya matumizi yao ajili ya kuwapatia mikopo nafuu kundi la vijana, wanawake na wenye ulemavu.

**UWEKEZAJI ULIVYO**

Mkurugenzi huyo anasema, wameshanunua pikipiki za bajaji 200 kwa ajili ya miradi kuwakopesha vijana wazitumie na kuacha kukaa vijiweni, mabasi madogo aina ya Toyota Coaster mbili zilizotolewa kwa baadhi ya vikundi na roli moja.

Pia Shauri anataja mradi wa jamii, kwamba inaendelea kujenga hospitali ya kisasa eneo la Kivule, machinjio ya kisasa (Vingunguti) ambayo anaamini yatakuwa mfano wa kuigwa.

Anasema wameshaanza ujenzi wa shule eneo la Mvuti, akifafanua: "Tunawajali watoto wa kike na tunafunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo tunawajali watoto wa kike na tunawajengea shule ya mfano ya watoto wa kike pekee."

Anasema Jiji la Dar es Salaam, kwa sasa lina uhaba wa walimu wa sayansi, lakini walimu wa masomo mengine wapo wa kutosha.

Hivyo, anasema kutokana na kutangazwa ajira mpya 6000 za walimu kitaifa, mkurugenzi huyo anaeleza imani yake kwamba, serikali itawapatia walimu wa sayansi.

Anasema katika kukabiliana na changamoto ya walimu wa sayansi, hivi sasa hawapokei kibali cha walimu wa masomo mengine kuhamia jijini Dar es Salaam, isipokuwa wa sayansi pekee.

"Tutawapokea walimu wa sayansi, wengine hatutawapokea, labda kama atakuwa na tatizo," anasema.

Pia katika miradi ya barabara, walipata fedha wastani wa Sh. bilioni 600 zilizosaidia kujengwa miradi hiyo ya barabara na katika awamu ya pili, wameomba fedha za kujenga kilomita 150, kwa ajili ya sehemu mbalimbali za jiji.

**MALALAMIKO**

Shauri anasema katika eneo la taka bado kuna shida inayowakabili na hasa barabarani, wananchi bado uelewa wa utunzaji mazingira na kufanya usafi sio mkubwa.

Anasema watu hawatupi taka katika mapipa yaliyoandaliwa, watu wanatupa taka chini na hata wengine wanatubutu kuingiza miferejini na kusababisha kuziba, hasa mvua zinaponyesha.

"Tumenunua gari saba za kubeba taka. Kuna vizimba vya taka, lakini watu wasio waaminifu wanaiba mifuniko ya vizimba. Tumejipanga sasa tutaweka mifuniko ya zege," anasema.

Ni mkakati anaosema unaendana na maboresho ya dampo la Pugu, na kwa sasa imeshatengenezwa, mvua zikinyesha magari yanapita tofauti na awali ilivyokuwa.

Rai yake mkurugenzi huyo ni kwamba, mtu mmoja mmoja ajilinde kiafya na kimazingira, akikemea wanaotumia mwanya wa mvua 'kutapisha' vyoo vyao.

Anaeleza katikati ya jiji vizimba vilikuwapo vya kukusanya taka, lakini vimeibiwa na hadi sasa kuna mitaa michache haina ofisi kwa ajili ya shughuli za maofisa watendaji kata na mitaa.

Hata hivyo, wameshaombewa pesa za bajeti na wanatarajiwa kupata ofisi, kunachana na ofisi za kupanga.

Anasema katika bajeti waliomba fedha na zimepatikana hivyo watajenga ofisi iliwaache kufanya kazi katika nyumba za kupanga.

Shauri anawaambia wafanyabiashara wa eneo maarufu la Kariakoo, kwamba wapo wengi na wanatakiwa kujenga utamaduni wa kufanya usafi wa mazingira yao, badala ya kuacha uchafu waliosababisha unazagaa.

Mkurugenzi anasema walikuwa na mpango wa kushirikiana na kampuni kubwa waweke vibanda vinavyofanana, hali itakayoupa mwonekanno mzuri ukanda huo wa kibiashara.

Anataja changamoto nyingine, ni baadhi ya wafanyabiashara kuingia na kufanya biashara katika maeneo ya watembea kwa miguu.

Mkurugenzi anataja hatua yao kukabili ni utoaji elimu, ikiwamo kutowekwa vibanda maeneo ya watembea kwa miguu au wasifanye biashara barabarani na kuwapa usumbufu madereva.





# Wabunge wapata dawa watoto wa mitaani

Na Augusta Njoji, DODOMA

WABUNGE wameishauri Bunge na serikali kuangalia sheria zilizopo kama zinalinda haki na usalama wa mtoto ili kuondokana na tatizo la watoto wa mitaani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, alitoa ushauri huo jana alipokuwa akihitimisha mjadala katika semina ya wajumbe wa Kamati ya Huduma za Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na viongozi wa Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Semina hiyo iliandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Railway Children Africa ambalo linafanya kazi katika halmashauri 12 nchini.

Nyongo alisema baada ya kupokea taarifa kutoka kwenye shirika hilo kuhusu hali ya watoto, wamebaini tatizo hilo ni kubwa na ni vyema kuweka mikakati ya kukabiliana nalo ikiwamo kufanya mapitio ya sheria ili zilinde haki na usalama wa watoto. "Sisi wabunge tuangalie zile sheria za kuendeleza watoto kama ziko sawa sawa, endapo zitakuwa ziko sawa basi tuangalie katika suala la utekelezaji wa sheria ili watoto wasiwe wanazurura mitaani," alishauri.

Hata hivyo, alisema serikali ina kazi ya kuhakikisha Idara za Maendeleo ya Jamii zinafanya kazi yake ipasavyo na halmashauri zinatenga fedha kwa ajili ya ustawi wa watoto.

Awali, wakichangia katika kikao hicho, Mbunge wa Mbulu Mjini, Zacharia Issaay, alisema kuna haja ya bunge na serikali kuja na sheria ya kuzuia watoto wa mitaani ili jamii iwajibike kuwatunza.

Alisema watoto wengi wanatekelezwa mitaani wanatokana na sababu mbalimbali ikiwamo wengine kuzaliwa nje ya ndoa na hivyo wazazi kushindwa kuwapa malezi yanayostahili watoto wao.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk.Paulina Nahato, alishauri kuimarishwa kwa kitengo cha saikolojia kwa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kuwa chanzo cha watoto kuwa mtaani ni kutelekezwa na wazazi ambapo wengi wanakabiliwa na msongo wa mawazo.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwamtumu Zodo, alisema uwapo wa watoto wa mitaani katika ukanda wa Pwani unachangiwa na umaskini na talaka.

Awali, akitoa mada kwa wabunge, Meneja Ushawishi kutoka shirika hilo, Rose Kagoro, aliwaomba wabunge kupaza sauti ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ili kulinda haki na usalama wao.

Kagoro alisema kazi kubwa ya shirika ni kuhakikisha wanawafikia watoto waliopo mtaani kwa kuwapa mahitaji ya lazima, kuwaunganisha na familia na kuwapa ujuzi.

Hata hivyo, alisema ukatili majumbani na umasikini vimekuwa visababishi vya watoto kukimbilia mitaani na kukumbana na matatizo makubwa zaidi ya waliyoyaacha nyumbani. "Wakiwa mtaani wanakumbana na ukatili na kushirikishwa katika vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya na uhalifu kama vile wizi," alisema.

Meneja huyo alisema utafiti unaonyesha kuwa kuna watoto 10,595 mitaani ambapo walio chini ya miaka 18 ni 6,393 na wale wenye umri mkubwa kuanzia miaka 18 hadi 25 walikuwa 4,202.

Meneja huyo alisema asilimia 50 ya watoto wa umri wa kati ya miaka 13 hadi 17 wamepitia vitendo vya unyanyasaji wakiwa na familia zao na asilimia 100 walikupambana na kadhia hizo wakiwa mitaani.

Alisema kuanzia Aprili mwaka 2018 hadi Aprili 2021, watoto 1,605 wameunganishwa na familia zao na watoto waliookolewa na kupewa makazi ya muda ni 1,733 huku waliyopewa misaada ya vifaa vya shule ni 3,923, watoto walioendelezwa kupata ujuzi na kupewa mtaji 1,375 huku familia 811 zikiwezesha mitaji.



Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania (ERB), Mhandisi Prof. Ninatubu Lema, akiteta jambo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Joseph Malongo, katika ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa miradi kwa wahandisi jijini Dodoma juzi.
**PICHA: WUU**

# Profesa ataka Watanzania wachangamkie fursa SADC

Na Paul Mabeja, DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kutumia fursa za kibiashara, kiuchumi na ushirikiano wa kimataifa kwa nchi wanachama zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ili kujiletea maendeleo. Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akifungua kongamano la miaka 40 la SADC lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Prof. Mwamfupe, alisema kuwa umefika wakati sasa wanachama katika jumuiya hiyo kuangalia fursa zilizopo katika nchi mbalimbali wanachama na kuzichangamkia.

"Ni wakati sasa wafanyabiashara wetu waone fursa zilizopo kwenye jumuiya hii na kuzifanyia kazi ili kuletea maendeleo," alisema Prof. Mwamfupe.

Alisema katika nchi wanachama zipo fursa nyingi ambazo mataifa yananufaika nazo ikiwamo vyuo kupata wanafunzi kutoka katika mataifa mbalimbali.

"Wakati wetu sisi jumuiya hii tulikuwa tunaisoma tu katika vyuo vyetu lakini hivi sasa inatakiwa kuangaliwa kwa jicho la utofauti ili kutambua fursa nyingi zilizopo na kuzichukua ikiwa ni pamoja na kutoa wataalamu katika sekta mbalimbali," alisema.

Akizungumzia mchango wa Tanzania kwa SADC, meya huyo alisema kuwa wakati jumuiya hiyo inaanzishwa mwaka 1980 Hayati Mwalimu Julius Nyerere alikuwa ni mmoja wa waasisi.

"Lakini pia mtakumbuka hivi karibuni hayati Rais wetu wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, alikuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo kwa mwaka mmoja na katika uongozi wake alifanikisha Kiswahili kuwa lugha rasmi katika jumuiya hiyo," alisema Prof. Mwamfupe.

Alisema ipo haja ya kutolewa kwa elimu hasa kwa wananchi wa maeneo ya vijijini kuitambua jumuiya hiyo na kuelewa fursa zilizipo na kuzifanyia kazi. "Tunapoimba wimbo wa taifa inatupasa kuimba pia wimbo wa SADC, ili wananchi wa kawaida kule vijijini waitambue jumuiya hii na kuzielewa fursa zilizopo,"" alisema Prof. Mwamfupe.

Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Faustine Bee, alisema kuwa hivi sasa wananufaika na ushirikiano uliopo wa kitaalamu na nchi wanachama wa SADC.

Alisema wanazo progamu za kubadilishana wanafunzi na nchi ya Msumbiji ambao wamekuwa wakija nchini kujifunza mambo mbalimbali na wanafunzi wa UDOM kwenda huko pamoja na kupokea wanafunzi wengine kutoka mataifa kama Congo DR, Zambia, Comoro, Burundi na maeneo mengine.

"Changamoto iliyopo ni lugha kwani Msumbiji wanatumia Kireno na wanafunzi wetu wanatumia Kingereza na Kiswahili lakini malengo ya chuo ni ifikapo 2030, chuo kuwa katika nafasi 20 bora kwa kuwa na wanafunzi kutoka nchi mbalimbali wanachama wa SADC," alisema Prof. Bee.

# NMB yakabidhi gari la kwanza

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

BENKI ya NMB jana ilimkabidhi gari la kwanza katika Kampeni ya Bonge la Mpango inayoendeshwa na benki hiyo kwa Hadija Iddi, Mkazi wa Chamwino Ikulu mkoani Dodoma.

Hadija anakuwa mshindi wa kwanza katika zawadi kubwa zinazotolewa na NMB katika kampeni hiyo iliyoanza Februari mwaka huu.

Akikabidhi gari hilo aina ya Tata Ace, maarufu kirikuu, lenye thamani ya Sh. milioni 25, Kaimu Ofisa Mkuu Ukaguzi wa Ndani wa NMB, Benedicto Baragomwa, alisema kampeni hiyo inaendelea nchini kote na zawadi mbalimbali zinaendelea kutolewa.

Baragomwa alisema NMB inatoa zawadi kwa wateja wanaoendelea kufungua akaunti zao na kwamba mshindi wa jumla atajinyakulia gari la kifahari.

Alisema gari litakalotolewa ni Toyota Fortuner lenye thamani ya Sh. milioni 169 ambalo ni litakuwa 'zero' kilomita.

"Ndugu Watanzania, hapa ninamkabidhi Hadija ufunguo wa gari lake, kama mnavyoona ni jipya, lakini tunazo zawadi nyingi kwa wateja wetu wanaoweka akiba kuanzia Sh. 100,000 kwenye akaunti zao za NMB," alisema Baragomwa.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa gari lake, Hadija alisema hakuamini kilichotokea na kuwa hakuwa amepanga lakini ni mpango wa Mungu.

Hadija alisema gari hilo litamsaidia katika shughuli zake za kujiongezea kipato, akiwashauri Watanzania kuwekeza katika benki hiyo kwa kuwa ina manufaa makubwa.

"Nimeamini kuwa yanayozungumzwa ni kweli, nimekabidhiwa gari jipya, nimepewa ufunguo na kadi ya gari vikiwa kamili kabisa, kweli NMB ndiyo mpango mzima," alisema Hadija.

Katika hatua nyingine, Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mulozi, aliongoza droo nyingine kwa ajili ya washindi ambapo watu mbalimbali walipata fedha baada ya kushinda.

Droo hiyo ilifanyika NMB tawi la Chamwino Ikulu chini ya usimamizi wa viongozi kutoka bodi ya michezo ya kubahatisha.

Hadi jana, NMB ilikuwa imetoa zawadi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 145 zikiwamo fedha taslimu, pikipiki za miguu mitatu aina ya LIFAN 16 na gari.



## W/biashara waomba uboreshaji ulipaji kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA jijini Mbeya, wameomba serikali kuendelea kuboresha mazingira ya ulipaji kodi ikiwa ni pamoja na usahihi wa ukadiriaji wa kodi hizo ili wafanye kazi zao kwa uhuru na kujiongezea kipato.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao wa masoko ya Sido na Mwanjelwa walisema kwa sasa hali ya biashara imeanza kuimarika tofauti na ilivyokuwa awali ambapo ubabe ulikuwa unatumika kwenye ukusanyaji wa kodi hali iliyokuwa inawalazimu baadhi kufunga biashara zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Atupele Mwinuka alisema tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alipotoa maelekezo wa Mamlaka ya Mapato (TRA) akitaka kuboresha mazingira kwa wawekezaji na wafanyabiashara hali imeanza kuwa nzuri.

Alisema tangu maelekezo hayo yalipotolewa, maofisa wa TRA wamebadilika na hakuna unyanyasaji tena kwa wafanyabiashara na kwamba hata lugha inayotumika kwa sasa ni rafiki kwao na inahamasisha kulipa kodi.

"Tulikuwa tukiwaona maofisa wa TRA tunafunga biashara na kukimbia, na ilikuwa inasababisha ukwepaji mkubwa wa kodi, walikuwa wakifika Mwanjelwa wenzetu wanatuambia kwamba wameshafika hivyo mjiandae, lakini sasa hivi hata wakikukuta hakuna shida, kilichobakia sasa hivi ni ukadiriaji wa kodi ndio unatakiwa kuboreshwa," alisema Mwinuka.

Naye Sajo Mwambipile alisema kuna utitili wa kodi ambao pia wanaiomba serikali izipunguze na kuongeza walipa kodi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wanajiita ni machinga lakini uhalisia unaonyesha kuwa uwezo wao sio machinga bali ni wafanyabiashara wanaostahili kulipa kodi kama walivyo wengine.

"Serikali ingefanya mpango wa kuhakiki upya biashara ili walipakodi tuwe wengi na viwango vipunguwe, sasa hivi kuna watu wanajificha kwenye mwamvuli wa machinga, lakini biashara ziko vizuri kwa sasa hatukutani tena na vitisho vya maofisa wa TRA," alisema Mwambipile.

Hata hivyo, alisema biashara nyingi zimeyumba kutokana na mlipuko wa Virusi vya Corona na hivyo ni vizuri Serikali ikaangalia namna ya kuwapa nafuu zaidi wafanyabiashara kwenye ulipaji wa kodi.

# Wanakijiji Chunya wakiri kumdanganya Magufuli

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

ZAIDI ya wananchi 20 wa Kijiji cha Chalangwa wilayani Chunya wamekwenda katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya wakiwawakilisha wenzao kukiri kuwa walimdanganya aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli.

Katika maelezo yao mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, walisema kuwa Aprili mwaka 2019 wakati Rais Magufuli alipofika kijijini hapo, walimueleza kuwa kuna mwekezaji anayechimba madini kijijini hapo kwenye eneo lenye makaburi na vyanzo maji, hivyo anahatarisha usalama wao.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Salum Hussen, mkazi wa siku nyingi wa kijiji cha Chalangwa, alisema kuwa maelezo waliyoyatoa siku hiyo Mbele ya Rais hayakuwa na ukweli wowote na kwamba waliamua kusema uongo ili Rais awasaidie kumwondoa mchimbaji huyo kwa vile hakuwa mkazi wa kijiji chao.

Alisema kuwa baadhi ya wananchi wenzao waliamua kusema uongo mbele ya Rais Magufuli baada ya kushawishiwa na baadhi ya watu ambao hakuwataja, ili wawasaidie kumwondoa mchimbaji huyo kwa lengo la kutaka eneo analochimba libaki wazi kwa kuwa walilitaka walitumie wenyewe kuchimba dhahabu.

"Kuna watu walitushawishi pale kijijini tuwasaidie kumuondoa mchimbaji huyu kwenye eneo alake ili wao wachimbe dhahabu, walifanya hivyo wakiamini kuwa eneo hilo lina madini mengi yaliyoachwa na wazungu tangu enzi za ukoloni, na sisi tukakubali kuwasaidia kumtoa kwa kumchongea uongo kwa Rais Magufuli," alisema Hassan.

Alisema kuwa baada ya kumweleza Rais kuwa mchimbaji huyo anachimba kwenye eneo lenye makaburi na pia lina vyanzo vya maji, Rais Magufuli alimuagiza Waziri wa Madini kufuatilia leseni ya mchimbaji huyo na ikiwezekana aifute na kurejesha eneo hilo kwa wananchi wenyewe.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chalangwa, Thadeo Elias, alisema wananchi walioshawishiwa kumdanganya Rais na wao wakakubali walidhani kuwa mchimbaji huyo akiondolewa wao watanufaika zaidi na eneo hilo, lakini hali imekuwa kinyume chake.

"Baada ya sisi wananchi kumdanganya Rais, Mchimbaji huyo alisimamishwa kuendelea na uchimbaji kutokana na sababu zile ambazo wananchi walimueleza Rais, sasa hata wao wenyewe wameshindwa kutumia eneo hilo kutokana na sababu zile zile za uongo walizozisema mbele ya Rais na sasa wameona bora wakiri ili ikiwezekana mchimbaji yule arejeshewe eneo lake ili waendelee kunufaika kama zamani," alisema Elias.

Alisema kabla mchimbaji huyo hajasimamishwa alikuwa akitoa michango mbalimbali ya maendeleo ya kijiji na pia vijana walikuwa wakipata ajira kwake, lakini baada ya kusimamishwa hakuna manufaa zaidi na ndio maana wananchi wamegundua makosa yao na kuamua mchimbaji huyo arudi.

"Tulikaa mkutano Mkuu wa Kijiji, wananchi wenyewe wakaamua tufike kwa Mkuu wa Wilaya kumweleza ukweli ili ikiwezekana atusaidie kumrudisha mchimbaji huyo, na kwa kuwa wananchi wenyewe waliamua sisi kama viongozi tunatekeleza uamuzi wao na ndio maana leo tumefika hapa kwa Mkuu wa Wilaya tukiwa na wazee maarufu wa kijijini kwetu kukiri makosa yetu na kumuomba atusaidie," alisema Mwenyekiti huyo.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka alisema kuwa kama maelezo hayo ndio uamuzi wa wananchi wote wa kijiji cha Chalangwa, Serikali itayasimamia ili mradi tu wakiona hayavunji sheria.

Gazeti hili limemtafuta mchimbaji huyo, Joseph Mwazyele, ambaye alisema kuwa baada ya kuona wananchi hao wanamdanganya aliyekuwa Rais, Dk. Magufuli pamoja na maelekezo ya Rais, akimtaka Waziri wa Mdini kufuatilia, aliamua kumuandikia Waziri barua kumweleza namna ambavyo wananchi hao walimdanganya Rais.

Alisema hata hivyo, barua yake haikuwahi kujibiwa na badala yake alisimamishwa kuchimba eneo hilo ingawa leseni yake haikufutwa na kwamba bado anayo.



Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Daniel Kamwela (kulia), akikabidhi zawadi ya sabuni kwa Oliver Moses aliyejifungua katika Hospitali ya Wilaya hiyo, wakati wa ziara ya kukagua na kuangalia namna huduma za mama na mtoto zinavyotolewa, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Polisi yaanza kutekeleza maagizo ya Samia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa maagizo kwa Jeshi la Polisi nchini kukabiliana na matukio ya uhalifu ikiwamo ujambazi, jeshi hilo mkoani Mbeya limeanza kutekeleza maagizo hayo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, ameanza kutekeleza maagizo hayo kwa kukutana na wakuu wa Polisi wa Wilaya zote za Mkoa huo kwa ajili ya kupeana mikakati.

Kikao cha viongozi hoa kilifanyika juzi katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya ambapo kilihudhuriwa pia na maofisa wa vyeo mbalimbali wa Jeshi hilo.

Akizungumza na wandishi wa habari baada ya kikao hicho, Kamanda Matei alisema kabla ya kukutana na viongozi hao pia waliwasiliana na baadhi ya viongozi wa idara zingine ambao watashirikiana nao kwenye utekelezaji wa maagizo hayo.

Alisema waliwasiliana na waganga wakuu wa wilaya zote ili kushirikiana kwenye utekelezaji wa agizo la kuwatibu kwanza watu wanaopata ajali badala ya kusubiri Fomu ya Polisi namba tatu (PF3) kama alivyoagiza rais Samia.

Alisema hivi karibuni kuna majambazi yalikuwa yanapanga njama za kufanya uporaji kwenye soko la madini lililoko katika Kijiji cha Igundu wilayani Chunya lakini kabla hayajatekeleza uharifu huo yakadhibitiwa kwa ushirikiano kati ya Polisi na wanannchi.

Vilevile alisema katika Mkoa huo wamejitahidi kudhibiti ajali za barabarani kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo ya magari ya mizigo nay a abiria kupita kwa kusubiriana kwenye maeneo ya miteremko mikali ikiwemo Mlima Mbalizi, Igawilo na Mlima Nyoka.

Aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya Mkoa huo kushirikiana na Jeshi hilo kwenye udhibiti wa matukio ya uharifu ikiwemo kutoa taarifa mapema endapo watabaini uwepo wa watu wanaopanga njama za kufanya uharifu.

Nao baadhi ya wakuu wa Polisi wa Wilaya, walisema kikao hicho kiliwaongezea ari ya kufanya kazi ya ulinzi wa raia na mali zao na hivyo wakawahakikishia wananchi kuwa watakuwa salama.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya kipolisi Mbalizi, Debora Hokololo, alisema kikao hicho kilikuwa muhimu kwao kutokana na maeneo yao kutofautiana na hata matukio ya uharifu ambayo huwa yanatokea yanatofautiana.

Alisema baadhi ya wilaya ziko kwenye maeneo yenye shughuli za uchimbaji wa madini kama Chunya, zingine ziko kwenye mipaka na nchi jirani kama Kyela na hivyo hata ulinzi wake unatofautiana.



# Katazo Z'bar kusajili meli za kigeni latinga barazani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulipatia ufumbuzi tatizo la Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni na hivyo kuikosesha mapato serikali.

Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, alisema ni muda mrefu sasa tangu Zanzibar kusitisha huduma za utoaji wa leseni kwa meli za kigeni kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali za usafirishaji wa bidhaa.

Aliitaka Serikali kufanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu na Zanzibar kuendelea kutoa huduma za usajili wa meli za kigeni.

"Mheshimiwa Spika, hili suala la Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni linazihusisha serikali mbili... sasa wakati mwafaka wa kulipatia ufumbuzi suala hili na kuona Zanzibar inaendelea na juhudi zake za kufanya usajili," alisema katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia hotuba ya makadirio na matumizi ya wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, aliitaka serikali kufanya mawasiliano na wenzao wa Jamhuri ya Muungano na kulimaliza tatizo la Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni.

Alisema tatizo hilo linazungumzika kati ya pande mbili kwa lengo la kuiwezesha Zanzibar kuingiza fedha za kigeni za usajili wa meli.

"Mheshimiwa, wakati umefika suala la Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni, linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa pande mbili za jamhuri ya muungano wa Tanzania"alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Gavu, alisema suala la Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni limeanza kuzungumzwa na pande mbili kwa mapendekezo kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi.

Hata hivyo, alisema hana uhakika kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama wamekuwa wakihudhuria vikao hivyo na kuwasilisha mapendekezo ya suala hilo.

"Mheshimiwa, wakati nilipokuwa waziri suala hili linalifahamu tayari pande mbili zimetakiwa kutoa mapendekezo katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili sasa sijui kwa upande wa Zanzibar kama wapo makini kiasi gani," alisema.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeizuia Zanzibar kutoa vibali vya leseni kwa meli za nje zinazopeperusha bendera ya Tanzania baada ya kubainika kujitokeza kwa kasoro mbal mbali ikiwamo meli zilizopewa leseni zikijishughulisha na kusafirisha dawa za kulevya na silaha.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Zantel, Aneth Muga (katikati), akiwa na Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Zantel, Emmanuel Swai (kushoto) na Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Zantel Kanda ya Pemba, Said Masoud Ali, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Pasua Anga Ki Zantel 4G, katika viwanja vya Gombani Kongwe visiwani Pemba juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yadhamiria kutokomeza kichocho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, imesema imejipanga hadi kufikia mwaka 2030 kuhakikisha ugonjwa wa kichocho unatokomezwa.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Kaimu Waziri wa Wizara hiyo, Omar Said, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa jimbo la Kojani, Hassan Hamadi Omar, aliyetaka kujuwa mikakati ya kupambana na ugonjwa wa kichocho Pemba.

Waziri huyo alisema ugonjwa wa kichocho unaisumbua jamii wakiwamo watoto chini ya umri wa miaka 15, ambayo husababishwa na maeneo yenye mito.

Alisema kichocho husababishwa na mazalia ya konokono ambapo maambukizi yake husababishwa pia na watu kujisaidia haja kubwa na ndogo katika maeneo yenye mito.

Alieleza Wizara ya Afya kupitia kitengo cha maradhi yasiyopewa kipaumbele imeanza kuchukua juhudi za kuweka dawa katika maeneo ya mito wanayoishi konokono.

"Mheshimiwa, kwa zaidi ya miaka miwili sasa serikali inatekeleza mradi wa kupambana na maradhi ya kichocho ambapo juhudi zimechukuliwa kwa ajili ya kutokomeza konokono ambao ndiyo chanzo cha maradhi hayo," alisema.

Aliyataja maeneo ambayo yameathirika na ugonjwa wa kichocho kwa upande wa Unguja ni Mwera, Koani, Mahonda pamoja na Mfenesini na kwa Pemba ni Ziwani, Kojani, Wawi na Mkoani.

## Zantel sasa yazindua kampeni yake upya

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Zantel, imezindua upya kampeni yake ijulikanayo kama 'Pasua Anga Ki Zantel 4G' inayolenga kuwapa wateja elimu ya matumizi sahihi ya mtandao wa 4G kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi.

Kampeni hiyo inayohusisha shughuli mbalimbali za uelimishaji, ilisimama kwa muda kupisha mambo kadhaa ikiwamo mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika katika viwanja vya Gombani Kongwe visiwani Pemba, Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Zantel, Aneth Muga, alisema lengo kubwa ni kuhakikisha wateja wananufaika zaidi na matumizi ya intaneti mbali na matumizi ya mitandao ya kijamii.

"Leo tunafuraha kuwajulisha wateja wetu kuwa tumerudi tena na kampeni yetu hii mahsusi ili kuendelea kutoa elimu kwa wateja wetu juu ya manufaa mbalimbali yatokanayo na mtandao ulioboreshwa wa Zantel 4G," alisema Muga.

Aliongeza kuwa Zantel inaendelea kuboresha mtandao ili kwenda na kasi ya ulimwengu kidigitali, ikiwamo kufanya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ikiwamo minara mipya ya simu hasa kwenye maeneo ya vijijini ili kuwafikia watu wengi zaidi.

"Nia yetu ni kuendelea kuboresha mtandao wetu ili mawasiliano yapatikane Zanzibar yote kwa kasi ya 4G na kumuwezesha mtumiaji kupata mawasiliano bora na ya haraka," alisema Muga na kuongeza:

"Ni wazi kuwa kupitia simu ya mkononi tu unaweza kufanya mambo mengi sana kwa haraka na urahisi zaidi. Mfano, kukata tiketi za safari mbalimbali kama boti, kununua na kuuza bidhaa mbali popote ulimwenguni kwa muda mfupi,kupata elimu, kuwasiliana na ndugu jamaa na marafiki."

"Kwanza kabisa, kupitia intaneti ya 4G mteja wetu anapata spidi ya kasi ambayo inamuwezesha kufanya shughuli zake mtandaoni haraka na kwa urahisi zaidi. Hii inamfanya mtumiaji kupata taarifa kwa haraka zaidi tofauti na yule anayetumia 3G," alisema.

Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Zantel Kanda ya Pemba, Said Masoud Ali, alisema mpango ni kuhakikisha kila mtu anafikiwa na mtandao wa 4G ikiwamo kuwawezesha watu kupata simu za bei nafuu.

"Tumeleta simu ambazo zina uwezo wa 4G na tunaziuza kwa bei nafuu ambapo tunatoa punguzo hadi asilimia 5 pamoja n GB 2 bure... hii inasaidia kila mtu kupata mtandao wetu wa 4G," alisema Ali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MSAFIRI PAUL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0627/0034** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **KIDELEKO SEKONDARI** mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MAG/PS/A.24/39/A/VOL1**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MURAMZI AMRI KABANYWANYI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0304-0127** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia BUKOBA SEKONDARI mwaka 1976. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control **No. 9910823586768.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAHADI TWAIBU MDIMILAGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3724/0036** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MUHANGA mwaka 2015,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **PWA/KIB/RB/253230/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.150/2021**

**Ombi la RAJABU TYABA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu RASHID ANZURUNI RASHID**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 18/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe18/05/2021

**AFRIMAX ENTERPRISE LIMITED**
**P O BOX 65123**
**DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **SAGCOAT Centre** Limited,tutauza gari Land Cruiser Prado **DFP 4374** pamoja na samani za ofisi kama ifuatavyo.
Dar es salaam-Ridoch Motors jirani na Haidery plaza jumamosi tarehe 05/06/2021 simu 0788058064/0745489389

Iringa-(iring Retco)jumatano 09/06/2021 simu 0788058064/0745489389

Mbeya-(Soweto,jirani na kiwira motel) jumamosi tarehe 12/06/2021
Simu 0788058064/0755366977.
Mali zitauzwa kama zilivyo kuanzia saa 4:00asubuhi na kuendelea

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.153/2021**

Ombi la **BESTINA SIXTO MWANYIKA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **SIXTO MICHAEL MWANYIKA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **22/06/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 20/05/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GODMERCY DAMAS WOISSO,**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili **MC220CGP.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taafifa :
**MOS/TR/RB/964/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BUHIGWE**

**Kituo cha MANYOVU Mkoa KIGOMA**

**Shauri la ndoa Na. 1, 2021**

**Jina la mdai: PHILIPINA KASSIM**

**Jina la mdaiwa: EVARIST BOSCO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: EVARIST BOSCO**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba ANAOMBA TALAKA KUTOKA KWA MDAIWA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 3 Mwezi 6 Mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 6 Mwezi 5 Mwaka 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Moshi kituo cha Uchira mkoa Kilimanjaro.**

**Usimamizi wa mirathi Na. 5/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU Chediel Filipo Mnandi wa Moshi.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA Alex Philipo Mbwambo**

**TANGAZO**

***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/masilahi yoyote ya mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi 06 mwaka 2021kabla huyo muamboji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia,**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 19 mwezi 5 mwaka 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo……...MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………….72…………2021**

**Ombi la……………CHANGWE MBWANA CHANGWE………...Kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi ya marehemu …..KUBO MBWANA CHANGWE…….**

**Kwa YEYOTE TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 26/5/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 18/5/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo ….MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………….14…………2021**

**Ombi la…..................... NAZARY PAUL MASSAWE……..Kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi ya marehemu …..NAZARI NAZARI MASSAWE….**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/6/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 19/5/2021

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/06/2021 SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA MAGARI AINA YA **NISSAN X-TRAIL T 689 CAC MALI YA DASTAN NGEMELA KABYEMELA, SUZUKI GRAND VITARA T 927 CBY MALI YA RICHARD WILLIUM MWAMBEJE NA NYUMBA MOJA ILIYOPO MPAMAA KARIBU NA KIGANGO CHA KANISA KATOLIKI MALI YA IDRISA MWENDI** BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MIKOPO WALIOKOPA **HERITAGE MICROFINANCE COMPANY LTD DODOMA.**

HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.MNADA HUO UTAFANYIKA KATIKA OFISI ZA HERITAGE MICROFINANCE COMPANY LTD KARIBU NA MPWAPWA FLATS.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/06/2021 SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA GARI AINA YA **SCANIA T 458 CEP MALI YA EMMANUEL LOMWALD CHAMBULILA NA BAJAJ RE 4S MC 678 AXN MALI YA JAFARI WAZIRI MATINDI** BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MIKOPO WALIOKOPA **HERITAGE MICROFINANCE COMPANY LTD DODOMA.**

HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.MNADA HUO UTAFANYIKA KATIKA OFISI ZA HERITAGE MICROFINANCE COMPANY LTD KARIBU NA MPWAPWA FLATS.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRESH FARMILY FOODS LTD**
Wanatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili
**T 791 DCB SCANIA.**
CHASSIS NO
**ys2pax2z0116029.**
ENGINE **NO 5333416.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi.Taarifa ya Polisi
**ARU/ARU/RB/251109/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MELCHIOR GODFREY SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili
**T 588 BUZ SUZUKI.**
CHASSIS NO **da62v315279.**
ENGINE NO **k6a2v315275**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi.Taarifa ya Polisi:
**ARU/ARU/RB/251162/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUSNA SALUM HASHAM**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.743 DKK**, aina ya IST iliyopotelea Kagongwa.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,
Taarifa ya jeshi la polisi,
**KAH/RB/TR/899/2021.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Imamu wa pili auawa DRC kipindi cha mwezi mmoja

**Beni,** DRC

LICHA ya kuanza kutumika kwa hali ya dharura kwa wiki mbili katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri, imamu mwingine anayepinga vikali msimamo mkali wa kidini, ameuawa katika eneo la Beni.

Djamal Moussa, ambaye ni kiongozi wa shirika la kiraia katika mji wa Mavivi, aliuawa kwa kupigwa risasi nyumbani kwake.

Atakuwa imamu wa pili kuuawa katika mwezi huu wa Mei katika eneo la Beni peke yake.

Kulingana na Donat Kibwana, Mkuu wa Wilaya ya Beni, Jamhuri ya Kodemokrasia ya Congo (DRC), Djamal Moussa, aliuawa kwa kupigwa risasi nyumbani kwake na mtu asiyejulikana baada ya kutoka kushiriki swala ya jioni.

Muuaji alimlenga kichwani kabla ya kutimkia msituni.

Karibu kilomita 10 kutoka jiji la Beni, huko Mavivi, imamu huyo alikuwa ni mwenye ushawishi na alikuwa ni mtu anayesikilizwa katika jamii yake ndogo.

Alionya mara kadhaa waandishi wa habari na mamlaka juu ya harakati na dhuluma zinazofanywa na kundi la waasi wa Uganda wa ADF katika eneo hilo.

Shehe Ali Amini aliuawa kwa kupigwa risasi wakati wa swala ya Magharibi, alikuwa imam wa kwanza kuuawa katika eneo la Beni mwezi huu wa Mei.

Kiongozi huyo alikuwa akikemea vitendo vya wanamgambo wa kiislamu kwenye eneo hilo, shirika la habari la Reuters liliripoti.

**RFI**



Wapalestina wakipita jirani na zilikoathirika nyumba baada ya mashambulizi ya angani yaliyofanywa na Israel eneo la Gaza. Kwa takribani wiki mbili Israel na Palestine wameendelea na mashambulizi na kusababisha zaidi ya vifo 200. **PICHA: XINHUA**

# Israel, Hamas zakana kusitisha mapigano

**Ukanda wa Gaza,** GAZA CITY

ISRAEL na Hamas wamekanusha kwamba kuna mipango ya usitishwaji wa mapigano kati yao hivi karibuni, wakati shinikizo linazidi.

Makabiliano baina ya pande hizo mbili yameingia siku yake ya tisa jana.

Izzat al-Rishak ambaye ni mwanachama wa ngazi ya juu wa Hamas, kundi linaloutawala Ukanda wa Gaza, alisema kuwa hakujawa na makubaliano yoyote ya kusitisha mapigano na Israel.

Televisheni moja ya Israel, awali iliripoti kuhusiana na uwezekano wa kusitishwa mapigano kuanzia kesho saa tisa alfajiri. Kulingana na ripoti ya Israel nayo imekanusha uwezekano wa mapigano kusitishwa.

Hayo yanakuja wakati Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu akisema operesheni ya kurusha mabomu Gaza inalenga kuwanyamazisha Hamas.

"Kuna njia mbili tu za kukabiliana nao, unaweza kuwashinda na hilo linawezekana au unaweza kuwanyamazisha na sasa tunawakabili kwa nguvu, lakini naweza kusema hatuondoi uwezekano wowote, tunatarajia tutarudisha utulivu kwa haraka.

"Tunafanya hivyo kwa makini ili tusiwaumize raia."

Taarifa zilielezea kuwa Rais wa Marekani Joe Biden, alizungumza na Netanyahu, na kumweleza kuwa, anatarajia kuona uhasama ukisitishwa.

Hali kadhalika, jeshi la Israel lilisema limeyashambulia kwa mabomu maeneo kadhaa nchini Lebanon, kujibu mashambulizi ya roketi yaliyorushwa kutoka maeneo hayo.

**DW**

# EU yafungua mipaka yake kwa wenye chanjo corona

**Brussels,** UJERUMANI

RIPOTI kutoka Umoja wa Ulaya (EU), zinaripoti kwamba nchi wanachama wa umoja huo, zimekubaliana jana, kufungua mipaka ya nchi zao kwa wasafiri ambao wamechomwa chanjo kamili dhidi ya virusi vya corona.

Katika mkutano mjini Brussels, wanadiplomasia wa nchi hizo walikubaliana kuongeza kiwango cha maambukizi ambacho kwa nchi iliyofikia itatangazwa kutokuwa salama.

Hatua hiyo inatarajiwa kutoa nafasi ya watu kuingia katika nchi za Umoja wa Ulaya kutoka nchi zengine.

Tangu Machi mwaka jana, usafiri usio na sababu za lazima katika nchi EU, ulipigwa marufuku, isipokuwa katika nchi chache tu zinazochukuliwa kuwa salama kutokana na idadi yake ndogo ya maambukizi.

**DW**

# Sita wafariki ghasia gereza Guatemala

**Cantel,** GUATEMALA

WATU sita wameuawa katika gereza moja lililopo Magharibi mwa Guatemala, baada ya ghasia kuzuka katika kituo hicho, viongozi walisema katika taarifa.

Waathiriwa walikutwa wamekatwa vichwa katika gereza lililojaa wafungwa wengi katika mji wa Cantel, katika jimbo la Quetzaltenango, kulingana na taarifa ya polisi.

Chanzo cha polisi, ambacho hakikutaka jina lake litajwe, kilisema mauaji hayo yalikuwa sehemu ya makabiliano kati ya makundi mawili hasimu yanayofanya biashara haramu ya dawa za kulevya.

Polisi ilidai kuwa imerejesha hali ya utulivu katika gereza hilo.

Jela hili lina wafungwa kutoka makundi mawili hasimu Mara Salvatrucha na Barrio 18, pamoja na wafanyabiashara wa dawa za kulevya, shirika la habari la AFP limeripoti.

**RFI**

# Viumbe vamizi huigharimu Afrika kiasi cha dola tril. 3.5

**Accra,** GHANA

UTAFITI mpya unasema wadudu, minyoo, mimea vamizi ya magugu, vinagharimu Afrika zaidi ya dola 3.5 trilioni, kila mwaka.

Watafiti walio Ghana, Kenya, Uingereza na Uswizi walielezea athari mbaya za spishi zinazoletwa na shughuli za wanadamu.

Nigeria, ambayo hasara yake inakadiriwa kuwa dola trilioni moja kwa mwaka, ni nchi iliyoathirika zaidi.

Gharama nyingi zinatokana na kupalilia, kazi inayofanywa hasa na wanawake na watoto, ingawa uharibifu unaosababishwa na wadudu unakadiriwa kuwa karibu na thamani ya dola bilioni 40.

**BBC**



# RAIS ATLETICO AMTAMANI GRIEZMANN




**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo amemkaribisha Antoine Griezmann kurudi katika klabu hiyo, ingawa hatarajii kama Barcelona wataweza kumuuza mchezaji huyo ambaye hajawa na wakati mzuri kule Camp Nou.

Griezmann alijiunga na Barca Julai, mwaka 2019, mwaka mmoja baada ya uvumi mkubwa kuhusu majaliwa yake.

Kwa kipindi cha miaka miwili kule Barca, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amefunga mabao 34 kwenye mechi 98 katika mashindano yote.

Msimu wake wa pili umeonekana kuimarika (akifunga mabao 19, ikilinganishwa na 15 kwa msimu wa kwanza).

Huku akiwa ameanza katika mechi 44 chini ya Ronald Koeman kwa msimu wa 2020-21, Griezmann ametolewa mara 27.

Hata hivyo, Cerezo hana shaka kuhusu ubora wa fowadi huyo, ingawa kurudi pale Wanda Metropolitano inawezekana ikawa ngumu.

"Ni mchezaji wa aina yake, lakini sidhani kama Barca wanataka kumuuza Griezmann," alisema rais wa Atleti akinukuliwa na Cadena SER.

"Nafikiri timu yoyote inataka kuwa na mchezaji kama Griezmann.

"Alikuwa na misimu ya kuvutia na sisi na nafikiri alikuwa mchezaji bora zaidi kwa Atletico Madrid."

## MULLER, HUMMELS WAREJESHWA UJERUMANI

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller na Mats Hummels wameitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ujerumani kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

Fowadi wa Bayern Munich, Muller na mlinzi wa Borussia Dortmund, Hummels hawajaichezea timu hiyo tangu Novemba, mwaka 2018.



Walikuwa ni miongoni mwa wachezaji wenye uzoefu ambao waliondolewa na Kocha Joachim Low na wakatolewa kwenye hatua ya makundi katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018.

Lakini wawili hao wameaminiwa tena na Ujerumani kwa ajili ya michuano hiyo ambayo itakuwa ya mwisho kwa Low kukinoa kikosi hicho.

Ujerumani ipo kundi moja na Ufaransa, Ureno na Hungary kwenye michuano hiyo ambayo iliahirishwa kufanyika mwaka jana kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mchezo wao wa kwanza katika Kundi F utakuwa dhidi ya Ufaransa katika dimba la Allianz Arena, Juni 15, mwaka huu.

Muller amekuwa na msimu wa kuvutia na alikuwa moja ya nguzo kubwa kwa Bayern kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ujerumani.

Kikosi kamili: Bernd Leno (Arsenal), Manuel Neuer (Bayern Munich), Kevin Trapp (Eintracht Frankfurt); Matthias Ginter (Borussia Monchengladbach), Robin Gosens (Atalanta), Christian Gunter (Freiburg), Marcel Halstenberg (RB Leipzig), Mats Hummels (Borussia Dortmund), Lukas Klostermann (RB Leipzig), Robin Koch (Leeds United), Antonio Rudiger (Chelsea), Niklas Sule (Bayern Munich); Emre Can (Borussia Dortmund), Serge Gnabry (Bayern Munich), Leon Goretzka (Bayern Munich), Ilkay Gundogan (Manchester City), Joshua Kimmich (Bayern Munich), Toni Kroos (Real Madrid), Florian Neuhaus (Borussia Monchengladbach); Kai Havertz (Chelsea), Jonas Hofmann (Borussia Monchengladbach), Thomas Muller (Bayern Munich), Jamal Musiala (Bayern Munich), Leroy Sane (Bayern Munich), Kevin Volland (Monaco) na Timo Werner (Chelsea

## FERNANDES: NATAKA TUZO NYINGI ZAIDI

**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes anataka tuzo binafsi zaidi baada ya kutajwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Manchester United kwa msimu wa pili mfululizo.

Fernandes amefuata nyayo za nyota wa zamani wa United, Cristiano Ronaldo na Ruud van Nistelrooy baada ya raia huyo wa Ureno kuwa mchezaji wa tano kwenye historia ya United kushinda tuzo hiyo mfululizo.

Fernandes alitwaa tuzo hiyo ya Sir Matt Busby Jumanne baada ya kupata asilimia 63 ya kura kutoka kwa mashabiki, akimzidi Luke Shaw ambaye alishika nafasi ya pili kwa kupata asilimia 21.

Alipoulizwa umuhimu wa tuzo hiyo, alisema: "Nyingi. Mara zote nimesema kwamba tuzo binafsi ni nzuri zaidi kwa wachezaji.

"Inakufanya uwe na hamasa zaidi, ni muhimu zaidi kwa mchezaji, lakini ni muhimu zaidi kupata taji ukiwa na timu.

"Kupata tuzo binafsi inaonyesha namna gani ulivyofanya mambo mazuri kwa timu, na ninaamini itanipa molari zaidi kwa ajili ya msimu ujao."

HABARI MICHEZO




# SOLSKJAER

## ASISITIZA ANAHITAJI STRAIKA

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekataa kuondoa uwezekano wa kumsajili straika wa Tottenham, Harry Kane na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

United imemwongeza mkataba mpya mshambuliaji wake, Edinson Cavani kwa msimu mmoja zaidi na alifunga bao kwenye mchezo wa sare ya 1-1 na Fulham, Jumanne.

Licha ya Cavani kusaini mkataba mpya, Solskjaer amefunguka kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji na kumsajili Kane, ambaye ameripotiwa kwamba anataka kuondoka kule Tottenham mwishoni mwa msimu huu.

"Ndio Edi (Cavani) amesaini mkataba mpya, lakini ni mastraika wangapi tupo nao klabuni hapa," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Siwezi kusema kwamba hatutasajili mshambuliaji. Bila shaka yoyote tunataka kuijenga timu.

"Naamini hadi mwisho wa msimu huu tutajua nini kitakachofanyika, lakini tunahitaji kuboresha safu ya ushambuliaji.

"Hivyo kuna uwezekano tukasajili washambuliaji wawili au zaidi na itategemeana na hali jinsi itakavyokuwa."

## MBAPPE ATAKA KUCHEZA OLIMPIKI

**PARIS, Ufaransa**

STRAIKA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amesema ana ndoto ya kuichezea Ufaransa kwenye michezo ya Olimpiki inayokuja ambayo itafanyika jijini Tokyo nchini Japan.

Mbappe na Ufaransa wanajiandaa na michuano ya Euro 2020, ambayo itafanyika mwezi ujao.

Wakati kikosi hicho cha kocha, Didier Deschamps kikiwa kwenye mipango ya kuhakikisha kinashinda taji la Euro, Mbappe kwa upande wake anataka kuichezea nchi hiyo kwenye michezo wa Olimpiki itakayoanza Julai mwaka huu.

"Kwa upande wangu, kutambulika kwenye nchi nzima ni muhimu sana," amesema Mbappe mwenye umri wa miaka 22 akiiambia TF1.

"Kila mmoja anajua kwamba, ndoto yangu ni kucheza kwenye michezo ya Olimpiki na nina matumaini nitaweza kutimiza ndoto yangu."

Katika michezo hiyo ya Olimpiki, Ufaransa ipo Kundi A pamoja na Japan, Mexico na Afrika Kusini.

# GUARDIOLA AMKATAA KANE

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amekataa kuhusishwa na uvumi wa kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane.

Kane ameripotiwa kwamba anataka kuondoka Tottenham, huku uvumi ukibainisha kuwa City, Manchester United na Chelsea zinawania saini yake.


Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo wa Jumanne dhidi ya Brighton and Hove Albion, Guardiola alikanusha uvumi huo.

"Swali linalofuata," alisema Guardiola baada ya mchezo huo wakati alipoulizwa kama atamsajili Kane mwishoni mwa msimu huu.

"Yeye ni mchezaji wa Tottenham Hotspurs, siwezi kuzungumzia kuhusu wachezaji wa timu nyingine."

Kane mwenyewe alinukuliwa mapema wiki hii akisema anahitaji kuondoka Spurs ili kwenda kutafuta changamoto mpya na kutafuta mataji.

City italazimika kuingiza sokoni kusajili fowadi mpya kwa sababu Sergio Aguero atandoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu baada ya mkataba wake kufikia mwisho.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE FURAHA TELE KUELEKEA EURO 2020

**Ni baada ya ndoto yake ya kucheza na Benzema aliyerejeshwa katika kikosi cha Ufaransa...**

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amefurahia kupata nafasi ya kucheza pamoja na Karim Benzema kwenye michuano ya Euro 2020, akibainisha kuwa hakuna wachezaji wengi bora kama mshambuliaji huyo wa Real Madrid.

Benzema mwenye umri wa miaka 33, Jumanne aliitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha Ufaransa baada ya kipindi cha miaka mitano, wakati alipojumuishwa na kocha, Didier Deschamps kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

"Nina furaha kubwa. Mara zote nilisema kwamba, nataka kucheza na wachezaji wakubwa," alisema Mbappe akiwaambia waandishi wa habari

"Benzema, sijawahi kucheza nae. Hakuna wachezaji wengi kushinda yeye. Atatuletea vitu vingi.

"Amecheza kule Madrid kwa miaka 10, ana uzoefu wa kushoto ni mchezaji mzuri nina uhakika atazoea mapema.

"Uzoefu wake utaisaidia timu kufanya vizuri zaidi na nina imani kubwa kwamba ataweza kuwa msaada kwa kikosi cha Ufaransa kwenye michuano ya Euro."

Benzema amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kule Madrid akifunga mabao 20 msimu huu kwenye Ligi Kuu Hispania, Laliga.

## KWA UFUPI

**KANE AICHAGUA CITY**

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 amesema anataka kuhamia Manchester City huku akiendelea kusukuma juhudi za kuondoka katika klabu ya Tottenham mwishoni mwa simu huu.***(Times)***

**NYOTA UNITED KUUZWA**

MANCHESTER United iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 25, pamoja na Jesse Lingard - ambaye yuko kwa mkopo West Ham kama sehemu ya kupata fedha za kumsajili Harry Kane. ***(Football Insider)***

**INGS ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United huenda ikawasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Southampton na England, Danny Ings mwenye umri wa miaka 28 mwishoni mwa msimu huu. ***(Telegraph - subscription required)***

**CHELSEA YAMTAKA SANCHO**

CHELSEA imetoa ofa ya pauni milioni 80 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England na Borrusia Dortmund, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21. ***(Sun)***

**HENDERSON AGEUKA LULU**

KLABU za Tottenham Hotspur, Chelsea, Borussia Dortmund na AC Milan zipo kwenye mbio moja kuwania saini ya golikipa wa England, Dean Henderson kutoka Manchester united. ***(Sky Sports)***

**LIVERPOOL YAMFUATA RAMSEY**

KIUNGO wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey anakodolewa macho na Liverpool ili kumsajili mwishoni mwa msimu huu. ***(Tutto Juve)***

**FLICK SAFARI IMEIVA**

KOCHA wa Bayern anayeondoka, Hansi Flick mwenye umri wa miaka 56, ambaye anahusishwa na kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani, anatakiwa na Barcelona kwenda kuchukua mikoba ya Ronald Koeman. ***(RAC1)***

**GRIEZMANN KUUZWA**

KLABU ya Barcelona ipo tayari kusikiliza ofa ya kumnunua, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30. ***(Marca)***

**BELOTTI KUTUA ROMA**

AS Roma ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia na Torino, Andrea Belotti mwenye umri wa miaka 27. ***(Calcio Mercato)***

**ARSENAL, EVERTON VITANI**

KLABU za Everton na Arsenal zimamfuatilia beki wa Real Betis, Emerson Royal mwenye umri wa miaka 22 raia wa Brazil, ambaye anacheza kwa mkopo kule Barcelona. ***(Sport)***



## HABARI MICHEZO

# UFUKWENI YAELEKEA AFCON NA MATUMAINI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 14 cha Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni kimeondoka nchini leo alfajiri na kuelekea Senegal kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (BSAFCON 2021) ikiwa na matumaini ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

Fainali hizo zinatarajia kufanyika katika Jiji la Dakar, kuanzia keshokutwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Mario Ndimbo alisema kikosi kimejianda vizuri na kipo tayari kwa ajili ya kushindana na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea.

Ndimbo alisema kikosi hicho kimefanya maandalizi mazuri na wanaamini wataonyesha ushindani kwa kupata matokeo chanya kama ambavyo inatarajiwa na wadau wengi wa mchezo huo.

"Kikosi cha Timu ya Taifa ya Ufukweni kinaondoka kesho (leo) alfajiri kuelekea Senegal, kiko tayari na kamili kwa ajili ya kwenda kupambana, tumeshawajua wapinzani wetu katika michuano hiyo ya BSAFCON, hatutaki kuwaangusha Watanzania," alisema Ndimbo.

Aliwataja wachezaji wa timu hiyo waliondoka ni pamoja na magolikipa watatu ambao ni Ahmed Juma, Adam Oseja, Shabani Kado wakati mabeki ni Eric Mayama, Rolland Msonjo, Said Moradi na Daniel Mwainyekule huku safu ya mastraika ikiwa na Kadhiru Said, Jaruph Juma, Yahya Tumbo, Abdulkadir Tabib, Ahmada Ahmada na Stephano Mapunda.

Katika fainali hizo, Tanzania ambayo inafundishwa na beki wa zamani wa Simba, Boniface Pawasa iko katika Kundi A ikiwa na Uganda pamoja na wenyeji Senegal.

Kikosi hicho cha Tanzania kitacheza mechi yake ya kwanza Jumapili dhidi ya Uganda na Mei 26, mwaka huu itawakabili Senegal.

Timu mbili zitakazofanya vizuri katika mashindano hayo zitakata tiketi ya kuiwakilisha Afrika kwenye fainali za Kombe la Dunia ambazo zitafanyika nchini Urusi baadaye mwaka huu.

Tanzania ilikata tiketi ya kushiriki fainali hizo zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa mara ya kwanza baada ya kuifunga Burundi jumla ya mabao 12-9, ikicheza mechi zote mbili kwenye ufukwe wa Coco hapa jijini kufuatia wapinzani wao kutokuwa na uwanja wenye sifa za michuano hiyo.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-bet Tanzania, Allen Mushi (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa mchezo wa Perfect 12, Juma Ngua (katikati). Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Michezo ya kubahatisha wa Mamlaka ya Mapato wa Mkoa wa kodi wa Ilala, Shaaban Mwanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shabiki wa Simba ashinda M-BET

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wawili wa soka hapa nchini wamejishindia zawadi ya jumla ya Sh. milioni 145. 9 baada ya kubashiri kwa usahihi zaidi ya mechi 12 katika mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12 unaochezeshwa na Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya M-Bet Tanzania.

Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, amewataja washindi hao ni Juma Makongo ambaye ni mkazi wa Mwananyamala jijini Dar es Salaam na Juma Mussa Ngua kutoka mkoani wa Singida.

Mushi alisema washindi hao kila mmoja alitumia Sh. 1,000 tu katika kubashiri mechi hizo 12 za ligi mbalimbali hapa duniani na kufanikiwa kugawana kiasi cha fedha hicho.

Alisema Makongo na Ngua wanakuwa washindi wa nane tangu kuanza kwa mwaka na kampuni yao ambayo imeshatumia zaidi ya Sh. milioni 550 kuwazawadia washindi mbalimbali waliobashiri kwa usahihi.

Ngua ambaye ni shabiki wa Simba alisema hakuamini kupata kiasi kikubwa cha fedha ambacho kitamsaidia yeye pamoja na wazazi wake na vile vile anajipanga kuanzisha biashara.

"Mimi ni mmachinga, sikutegemea kupata kiasi kikubwa cha fedha, nitaanza kujenga nyumba ya wazazi wangu huku nikiboresha biashara," alisema Ngua.

Mkuu wa Kitengo cha Michezo ya kubahatisha wa Mamlaka ya Mapato wa Mkoa wa kodi wa Mkoa wa Ilala, Shaaban Mwanga aliipongeza M-Bet kwa kuwa walipa kodi wazuri hapa nchini.

## Serikali yafanya ukaguzi wa gym

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo Nchini (WMA), umefanya ukaguzi kwenye maeneo ya kufanyia mazoezi maarufu kama Gym ili kujua kama vifaa vinavyotumika vina vipimo sahihi vinavyokubalika kisheria.

Ukaguzi huo ulifanywa kwenye kumbi mbalimbali jijini Dar es Salaam kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Vipimo Duniani inayoadhimishwa kila Mei 20, ya kila mwaka na kuitaja kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa vipimo katika afya.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Kaimu Meneja wa WMA, Mkoa wa Kinondoni, Charles Mavunde, alisema kukagua vifaa vya mazoezi ni muhimu kwani bila kufanya hivyo vinaweza kuhatarisha afya za watu wanaofanya mazoezi hayo.

Mavunde alisemsa gym ni eneo ambalo WMA inatakiwa kuhakiki vyuma ambavyo wananchi wanatumia kuinua vyenye uzito mbalimbali kwani kabla ya kutumia wateja hivyo vyuma maofisa wa WMA lazima wapime kama uzito uliopo ni sahihi.

Alisema uhakiki wa vipimo hivyo ni muhimu ili mtu asije kutumia aidha uzito mkubwa sana au mdogo sana akashinwa kupata kile anachokihitaji.

## Polisi Tanzania yaongoza sare

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Bara ikielekea ukingoni, Polisi Tanzania ndio timu inaongoza kwa kuwa na sare nyingi mpaka sasa, ikiwa imeshatoka sare mara 14.

Timu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Polisi Tanzania na kutumia Uwanja wa Ushirika mjini Moshi na mara nyingine Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, imeshacheza mechi 30 mpaka sasa ikibakisha mechi nne tu ili kumaliza msimu huu wa 2020/21.

Maafande hao ambao wana pointi 41, wameshinda mechi tisa, wamepoteza saba huku wakitoka sare michezo 14.

Mbeya City inakamata nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu kwa kuwa na sare nyingi, ikiwa ina sare 12, nayo ikicheza mechi 30, ikishinda saba na kupoteza 11, timu hiyo kwa sasa inajipapatua kubaki Ligi Kuu, ikiwa kwenye nafasi ya 13 kwa pointi 33.

Yanga inayoshika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ikiwa na pointi 61 kama Simba, lakini ikizidiwa idadi ya magoli ya kufunga inazingoza timu zinazoshika nafasi ya tatu kwa sare nyingi.

Timu hiyo imepata sare 10 mpaka sasa, sawa na Prisons, Namungo na Gwambina FC ambazo zote zina idadi hiyo ya sare.

# Michezo

Ijumaa Mei 21, 2021

Nipashe



MBAPPE FURAHA TELE KUELEKEA EURO 2020

HABARI UK 22



Golikipa wa Simba, Aishi Manula akiruka kupangua mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuwakabili Kaizer Chiefs kutoka Afrika Kusini katika mchezo wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# YANGA - UBINGWA BARA TUTAUBEBA

## ●●●Yafunguka imerejea katika mbio za kuwania taji hilo na imejipanga kuendeleza...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata pointi tatu muhimu katika mechi dhidi ya JKT Tanzania hapo juzi, kikosi cha Yanga kimeanza kutamba kimerejea kwa 'kasi' katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu wa 2020/21 ambao tayari unaelekea ukingoni.

Kwa ushindi huo, Yanga ilifikisha pointi 61 sawa na vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, lakini wao wakicheza michezo minne zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Makipa wa Yanga, Razak Siwa alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kushinda katika kila mechi iliyoko mbele yao ili watimize malengo waliyokuwa nayo na hawajakata tamaa.

Siwa alisema ushindi walioupata katika mechi dhidi ya JKT Tanzania ulitokana na wachezaji kupambana katika muda wote na hatimaye walifanikiwa kuondoka na matokeo mazuri, jambo ambalo watalifanya kwenye michezo mingine iliyobakia.

"Matokeo ya mechi yetu na JKT Tanzania yamefufua imani yetu, bado tuko katika mipango yetu ya mbio za ubingwa, kila kitu ni mipango na tunapaswa kutulia na kuendelea kufanya vizuri, tutahakikisha tunapata pointi tatu katika kila mechi, bado tutapambana kutafuta ubingwa bila kuangalia nani tunacheza naye, jambo la msingi ni kuhakikisha tunashinda mechi zote," alisema Siwa.

Aliongeza benchi la ufundi linaendelea kuyafanyia kazi mapungufu waliyoyabaini kwenye kikosi chao ili kuwaimarisha wachezaji kwa ajili ya kuendelea na mapambano yanayowakabili.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa timu hiyo, Antonio Nugaz aliliambia gazeti hili wanachohitaji ni kupata ushindi kila mchezo na matokeo hayo yatawaweka kwenye mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa na si jambo lingine.

Nugaz alisema watapambana mpaka katika mchezo wa mwisho ambapo huko ndio watajua hatima yao kuelekea mbio hizo za kusaka ubingwa.

"Tumepata alama tatu. Hatumwangalii mtu, sisi tunacheza michezo yetu. Tukipata ushindi tunashukuru, sare au kufungwa yote tunashukuru Mungu, lakini sisi tutafanya hesabu mpaka mwisho wa ligi na si sasa," alisema Nugaz.

Aliongeza wao kama viongozi wameweka nguvu ya kupata ushindi katika mechi zote zilizobakia na hawajali nini kitatokea kwa sababu wao ni wapambanaji.

"Tumeweka nguvu kwenye michezo yetu ili tupate alama tatu. Nikwambie tu kuwa sisi ni wapambanaji na tutapambana hadi tone la mwisho, hatutokata tamaa," alisema kiongozi huyo.

Kikosi cha Yanga sasa kinaendelea na maandalizi ya kuwafuata Mwadui FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa Mei 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga.

## SIMBA YASISITIZA KESHO WATACHEKA

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mchezo wao wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chifes utakaochezwa kesho, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema ana matarajio makubwa kutoka katika kikosi chake na kwenye mchezo wa soka hakuna kisichowezekana.

Gomes aliliambia gazeti hili alifanya makosa katika mechi ya kwanza kwa kutumia viungo wawili ambao walikuwa wakiziba nafasi na kuwafanya wapinzani wao kucheza mipira ya juu.

Kocha huyo alisema tayari amefanyia kazi mapungufu ya kikosi chake na anatarajia watafanya vizuri katika mechi ya kesho endapo wachezaji wake watajitoa kwa kiwango kikubwa katika mchezo huo ambao wanahitaji 'kupindua meza'.

"Wao wametufunga kwao mabao 4-0 katika mchezo wa kwanza uliocheza Johannesburg wiki iliyopita, nakiri hatukucheza vizuri hasa kwenye safu ya ulinzi kitu ambacho benchi la ufundi limefanyia kazi kuondoa makosa yote, tunapaswa kupambana kiume, wachezaji, benchi la ufundi, viongozi pamoja na mashabiki tunatakiwa kujua kwenye mpira kila kitu kinawezekana na tunajiandaa kufanya vizuri," alisema Gomes.

Aliongeza wamejiandaa kuingia dimbani tofauti na walivyocheza ugenini na anawaondoa hofu mashabiki wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu waliruhusu kufungwa idadi kubwa ya mabao, lakini bado anaimani uwezo wa kulipa kisasi wanao.

Alisema Simba imejiandaa kufanya vizuri katika dakika 90 zilizobakia baada ya wapinzani wao kutumia vyema dakika 90 za kwanza za hatua hiyo ya robo fainali.

"Tuna imani na kujiaminisha kwamba tunaenda kupindua matokeo, kikubwa kila mmoja wetu anatambua umuhimu wa hii mechi tunakwenda kupambana na kupata matokeo mazuri na kusonga mbele," alisema Bocco.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002